SportPesa
TZS. 619,207,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**BoT yatangaza msako dhidi ya wachafuzi noti**

UKURASA 3



**Pogba akanusha kumtukana Solskjaer**

UKURASA 22

Nipashe
Ijumaa Oktoba 29, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580748
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## KESI YA MBOWE

# Patashika Kibatala, msaidizi wa Sabaya

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**AVEVA AFUNGWA KIFUNGO CHA NJE, KABURU HURU**

ALIYEKUWA Rais wa Klabu ya Simba, Evance Aveva amehukumiwa kifungo cha nje cha miezi sita baada ya...

UKURASA WA 4

**HOJA TANO ZA PAC KWA JESHI LA POLISI**

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imetoa maagizo matano kwa Jeshi la Polisi ikiwamo...

UKURASA WA 4

**UJERUMANI YAIPA TANZANIA BIL. 119/-**

SERIKALI ya Shirikisho la Ujerumani imeipatia Tanzania msaada wa Sh. bilioni 119.25 kwa ajili ya kuboresha...



Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, akiwa mwenye furaha, baada ya kushinda kesi ya madai ya kashfa dhidi ya Mhariri wa gazeti la Tanzanite, Cyprian Musiba, katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana na kutakiwa kulipwa fidia ya Sh. bilioni 6. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Musiba kumlipa Membe bil. 6/-

UKURASA 3

# Serikali yasitisha uhamisho wa watumishi mijini

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA SC MWENDO WA VISHINDO UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, wakitoka kusikiliza kesi inayowakabili ya uhujumu uchumi katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Patashika Kibatala, msaidizi wa Sabaya

**Na Kulwa Mzee**

WAKILI Peter Kibatala jana alikuwa katika patashika na shahidi wa Jamhuri, Justine Kaaya, ambaye juzi alidai alikuwa msaidizi wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Akimhoji shahidi huyo jana katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mbele ya Jaji Joackim Tiganga, Wakili Kibatala aliuliza kuhusu shahidi huyo kudai kufuatwa na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akiwa na gari aina ya Land Cruser V8 lenye bendera ya Bunge na mlingoti likiwa na namba KUB ilhali alishanyang'anywa na uongozi wa Bunge kabla ya Januari 2020.

Mbowe aling'anywa gari hilo na uongozi wa Bunge Septemba 2017, akiwa Nairobi alikokuwa akilitumia wakati Tundu Lissu akipatiwa matibabu.

Shahidi huyo wa pili alidai hafahamu kama Januari 2020, Mbowe hakuwa na gari hilo alilodai juzi kwamba lilimchukua Machame Road na kwenda Aishi Hotel, ambako walifanya kikao, akiombwa ataje majina ya marafiki wa Sabaya.

Akihojiwa na Kibatala kama marafiki wa Sabaya aliowataja ni viongozi wa serikali, shahidi huyo alidai hawakuwa viongozi wa serikali.

Alidai hafahamu kama Sabaya mhalifu, hafahamu kama alikuwa akifanya vitendo vya kihalifu kuanzia 2018 hadi 2020 akiwa Mkuu wa Wilaya ya Hai lakini akakiri taarifa za kufungwa miaka 30 jela alizisikia.

Wakili Kibatala alihoji kama shahidi huyo anafahamu namna taarifa za uhalifu za Sabaya zilivyoyofikia vyombo vya sheria hadi akashtakiwa na kama anafahamu Mbowe alitoa taarifa mara kadhaa za vitendo vya uhalifu wa Sabaya kwa Inspekta Jenerali wa Polisi, IGP Simon Sirro.

Shahidi alidai hafahamu kuhusiana na taarifa hizo, lakini anafahamu moja ya majukumu ya wabunge ni kukusanya taarifa za uhalifu na kutoa taarifa hizo kwenye vyombo husika.

Alidai Mbowe wakati anaomba taarifa za Sabaya alikuwa mbunge lakini hafahamu taarifa alizokuwa akizihitaji kwake alikuwa anazifanyia nini.

Kaaya alidai Mbowe hakusema anataka kuwadhuru marafiki wa Sabaya, hakusema kama anataka kumdhuru Sabaya na hafahamu kama taarifa hizo alizitafuta kwa ajili ya kuwatafuta watu waliomdhuru Mwenyekiti wa Hai.

Wakili Kibatala alihoji kama shahidi anafahamu Sabaya alizuiliwa kufika katika baadhi ya hoteli kama vile SG Resort kwa kuwa alikuwa akidaiwa Sh. milioni nane, Kaya akidai hafahamu.

Shahidi huyo alidai alilala Aishi Hotel lakini alikiri kwamba hakusema mahakamani namba ya chumba alicholala na hakutaja aina ya chakula alichokula katika hoteli hiyo.

Wakili Kibatala katika kujenga swali lake, alidai Januari 2020 ambayo shahidi anadai kukutana na Mbowe, kiongozi huyo wa CHADEMA na Esther Matiko (aliyekuwa Mbunge wa Tarime Mjini) walikuwa gerezani baada ya kufutiwa dhamana na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Novemba 23, 2019.

Shahidi alidai hafahamu kama walikuwa gerezani kisha wakaachiwa Machi 2020.

Shahidi huyo pia alidai namba zake za simu ni 0754 916666 na 0693006700 lakini namba iliyoandikwa katika maelezo yake, 0754216170, ikidaiwa kuwa yake haifahamu.

Alidai sio sahihi kwamba jina lake lingine ni Power Kaaya, alipewa kwa sababu ya uhalifu aliokuwa akiufanya maeneo ya Arusha na Longido.

Shahidi huyo alidai hafahamu kama Mbowe alikuwa mhalifu na taarifa alizokuwa anahitaji kutoka kwake pamoja na kufikiria kulikuwa na uhalifu ndani yake, hakuwahi kuziripoti polisi na fedha alizodai kupewa na Mbowe Sh. 300,000 na Sh. 200,000 alizipokea kwa kuwa alimwambia za usumbufu.

Pia alidai hakuwahi kuwaambia marafiki wa Sabaya kwamba Mbowe aliomba namba zao, akidai kuwa wakiwa gerezani, mshtakiwa Halfani Bwire na Mohammed Ling'wenya walimsimulia taarifa zao.

"Bwire alikuwa ananisimulia kuwa walimfuata Sabaya hadi Ikulu ndogo wakakurupushwa, aliniuliza kama mimi ndio niliwakurupusha.

"Yale tuliyokuwa tunasimuliana na Bwire sikuyaandika katika maelezo yangu, sikumbuki askari walionikamata Agosti 25, 2020 lakini kuhusu Bwire, Joyce Mukya, Mbowe nakumbuka," alidai shahidi huyo.

Shahidi alimaliza kutoa ushahidi wake na kesi iliahirishwa hadi leo kwa ajili ya shahidi wa tatu wa upande wa mashtaka kuanza kutoa ushahidi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanashtakiwa kwa mashtaka sita, yakiwamo ya kula njama kufanya vitendo vya kigaidi Arusha, Moshi, Mwanza, Morogoro na Dar es Salaam kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020.

# Serikali yasitisha uhamisho watumishi mijini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesitisha kwa muda uhamisho wa watumishi wanaotaka kuhamia kwenye majiji, manispaa na miji na kutangaza kipaumbele kitatolewa kwa wanaotaka kuhamia vijijini.

Hatua hiyo imetangazwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ambaye alitaja mambo mawili likiwamo la uhamisho kumnyima usingizi.

Waziri Ummy alikuwa akitoa taarifa kuhusu mapato na matumizi ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2021, ikiwa ni robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22.

"Ukiachana na masuala ya maendeleo nina kero kubwa mbili zinaninyima usingizi, vibali vya watu wanaotaka kuhama, bahati mbaya wengi wanaotaka kuhama wanataka kuhama kuja mijini, hakuna mtu nimemsikia anataka kutoka Tanga, Dodoma, Dar es Salaam, aende vijijini."

"Nimesimamisha uhamisho wa watumishi wote najua ni haki yao kuhama, lakini nimesimamisha kwa muda uhamisho wa watumishi waliochini ya TAMISEMI wanaotaka kwenda kwenye majiji, manispaa na miji, hadi tutakapojiridhisha," alisema.

Pia alisema ameangalia takwimu na kubaini halmashauri ya mji ina walimu 2000 huku za vijijini zina 200 na kushangaa wanaoruhusu wahame kwenda mijini.

"Leo kama kuna mtumishi wa TAMISEMI anataka kutoka Dodoma Jiji, Tanga Jiji, Temeke, Ilala, Kinondoni, Arusha, Mwanza, aende Mlele, Nsimbo, Momba huyo Katibu Mkuu hata leo mruhusu, kwa sababu tukisema mambo ya ndoa kila mtu ana familia tutahamisha wangapi? Kwa hiyo tunachambua kwanza vigezo ndiyo tutafungua tena uhamisho," alisema.

Alitaja kero nyingine ni madeni ya wazabuni zikiwamo halmashauri kudaiwa kwa kiwango kikubwa.

"Halmashauri zihakikishe zinalipa madeni yaliyohakikiwa ya wazabuni, watoa huduma na watumishi kwa sababu kuna madeni mengine yanalipwa na Hazina, lakini madeni mengi wanatakiwa kulipwa, kinachosikitisha unakuta tumepeleka fedha ya kujenga kituo cha afya hawamlipi mkandarasi na fedha inaisha."

"Siku hizi tuna mambo ya mkeka kwa hiyo tutatoa mkeka, je hii hela ilipelekwa halmashauri au haijapelekwa, hivyo naagiza uwekwe mpango wa kulipa madeni ya wazabuni na watoa huduma, inasikitisha kuna watu wameuziwa nyumba zao, wengine wameuziwa mashamba yao," alisisitiza.

Kadhalika, aliwaonya tabia ya kulazimisha wananchi kusomba mawe na vifusi kwenye ujenzi wa madarasa yanayojengwa kwa fedha za UVIKO-19 na kudai kuwa fedha zilizotolewa zimejumuisha gharama za mawe na mchanga.

"Hili suala liachwe, ushiriki wa wananchi ni muhimu hawapaswi kulazimishwa wala kunyang'anywa vitu, hatutategemea kusikia watu wananyang'anywa kuku wao kwa sababu ya ujenzi," alionya.

HABARI KITAIFA



Naibu Balozi wa Uingereza hapa nchini, Rick Shearn (katikati) na Mkurugenzi wa Maendeleo wa ubalozi huo, Kemi Williams (kulia), wakipokea maelezo kutoka kwa mfanyakazi wa kiwanda kipya cha kutengenezea pombe kali cha Serengeti Breweries Ltd (SBL), walipofanya ziara ya kikazi kiwandani hapo, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Musiba aamuriwa kumlipa Membe bil. 6/-

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imemhukumu na kumwamuru Cyprian Musiba kumlipa fidia ya Sh.bilioni sita aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Bernard Membe kwa kumchafua.

Hukumu hiyo imetolewa jana mbele ya Jaji Joacquine De Melo baada ya kupitia ushahidi wa mlalamikaji na kukubaliana na madai yake.

"Kesi hii inaamuliwa upande mmoja kwa sababu mlalamikiwa hakuwahi kuwasilisha utetezi, mahakama inakubali kwamba maneno yaliyotolewa na Musiba yalikuwa yanamchafua mlalamikaji.

"Mahakama inaamuru Musiba amlipe fidia ya Sh.bilioni sita Membe na inatoa zuio la kudumu, mlalamikiwa hatakiwi kuendelea kukuchafua, mahakama inamwamuru kulipa gharama za kesi, " alisema Jaji Melo.

Hukumu hiyo inatokana na shauri namba 220 la mwaka 2018 na kwa mara ya kwanza ilitajwa Februari 26, 2019.

Katika kesi hiyo Membe amemshtaki Musiba, Mhariri wa gazeti la Tanzanite na wachapishaji wa gazeti hilo akiwadai Sh. bilioni 10 kwa kumchafua.

Musiba katika kesi hiyo anashtakiwa kwa kumtuhumu Membe kuwa anamhujumu Rais John Magufuli asitekeleze majukumu yake ya kuwaletea wananchi maendeleo huku akidai kwamba mbinu mojawapo ya kukamilisha hujuma hizo ni maandalizi anayofanya kugombea urais mwaka 2020 kupitia CCM.

Hiyo ni kesi ya pili kwa Musiba kutakiwa kulipa fidia mwaka huu, kesi ya kwanza ilitolewa hukumu Agoti 11, mwaka huu katika Mahakama Kuu Zanzibar.

Mahakama hiyo ilimwamuru Musiba na gazeti la Tanzanite, kumlipa fidia ya Sh. bilioni 7.5 Wakili wa kujitegemea, Fatma Karume baada ya kubaini alimchafua kwa kumzushia taarifa za uongo.

Fatma alifungua kesi mwaka 2019 dhidi ya Musiba akilalamikia kuchafuliwa na mara ya kwanza ilitajwa Oktoba 3, 2019.

Katika madai yake Fatma alimlalamikia Musiba kumchafua kwa kumzushia taarifa za uongo zenye lengo la kushusha hadhi yake katika jamii.

Fatma alidai katika malalamiko yake kwamba Musiba alimwambia ametiwa mimba na muuza unga na kwamba hana staha wakati anadai maelezo hayo si kweli kwa kuwa ana mume na watoto.

# BoT yatangaza msako wanaochafua noti

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema itaanza kuwachukulia hatua watu watakaohusika na matumizi mabaya ya noti ikiwamo kuweka pesa sakafuni au sehemu yoyote ambayo si nadhifu.

Kwa mujibu wa BoT, hatua hiyo imetokana na kuibuka kwa baadhi ya wananchi kufanya matumizi mabaya ya noti katika shughuli mbalimbali za kijamii, hususani kwenye sherehe za harusi.

BoT imesema watu hao wamekuwa wakitunza wahusika kwa kuwarushia noti zinazoanguka sakafuni wakati mwingine kukanyagwa.

Taarifa iliyotolewa jana na Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, ilisema watu hao muda mwingine huvиringisha noti katika maumbo mbalimbali na kutumia kama mapambo na hata kuweka kwenye mwili wa mtu ulioloa jasho.

"Matendo haya yanatweza fedha ya Tanzania ambayo ni moja ya tunu za taifa letu. Vitendo hivyo vinaendelea kutokea licha ya Benki Kuu ya Tanzania na viongozi mbalimbali wa serikali kwa nyakati tofauti kuvikemea," alisema Prof. Luoga katika taarifa hiyo.

"Hivyo basi Benki Kuu ya Tanzania inatoa onyo kwa wananchi ambao bado wanakaidi onyo hili ambalo limetolewa mara kadhaa kuhusu namna sahihi ya kutunza noti za Tanzania zinazokuwa mikononi mwao kwa kuzituma kinyume cha maadili pamoja na matakwa ya kisheria," aliongeza.

Taarifa hiyo ilisema vitendo vya matumizi mabaya ya fedha vinachangia kutweza fedha ya nchi na kusababisha uchakavu, hivyo kuiongezea serikali gharama kubwa za kuchapisha fedha zingine.

"Aidha Benki Kuu inawashauri washiriki katika matukio yote ambayo yanahusisha matumizi ya fedha, kuandaa vyombo maalum vya kuweka fedha badala ya kufanya vitendo ambavyo havikubaliki," alisisitiza Gavana katika taarifa hiyo.

Kadhalika, taarifa hiyo iliwataka wananchi kutoa taarifa BoT au katika vyombo vya usalama pindi wanapobaini matumizi yasiyo sahihi ya fedha ili hatua za kisheria zichukuliwa dhidi yao.

# Aveva afungwa kifungo cha nje, Kaburu yu huru

**Na Hellen Mwango**

ALIYEKUWA Rais wa Klabu ya Simba, Evance Aveva, amehukumiwa kifungo cha nje cha miezi sita baada ya kupatikana na hatia ya matumizi mabaya ya madaraka.

Pia, mahakama hiyo imemwachia huru aliyekuwa Makamu wa Rais wa klabu hiyo, Godfrey Nyange maarufu kama Kaburu kutokana na ushahidi wa Jamhuri kushindwa kumtia hatiani dhidi ya tuhuma zilizokuwa zinamkabili.

Hukumu hiyo ilisomwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na Hakimu Mkazi Mkuu,Thomas Simba.

Akitoa hukumu hiyo alisema mahakama yake bila kuacha shaka upande wa Jamhuri imethibitisha mashtaka ya matumizi mabaya ya madaraka dhidi ya Aveva na kwamba mahakama yake inamtia hatiani.

"Mahakama yangu inamtia hatiani mshtakiwa wa kwanza Aveva dhidi ya matumizi mabaya ya madaraka atakwenda jela kutumikia kifungo cha nje cha miezi sita," alisema.

Akiichambua hukumu hiyo alisema hakuna ubishi kwamba Dola za Kimarekani 300,000 ziliingizwa kwenye akaunti ya Klabu ya Simba kupitia Benki ya CRDB ambayo ni mauzo ya mchezaji Emmanuel Okwi.

Alisema baada ya kuingia kwenye akaunti hiyo inaonyesha kwamba kamati tendaji ya klabu ya Simba ilielekeza itolewe fedha hiyo kwenye akaunti ya Simba ili itumike kwenye uwanja wa Bunju kujengwa kwa nyasi bandia.

"Ushahidi umethibitisha kwamba ile fedha ilitakiwa ijenge nyasi bandia kwenye Uwanja wa Bunju, lakini haikufanyika hivyo matokeo yake zilienda kwenye akaunti binafsi ya Aveva, kinyume cha maelekezo ya kamati hiyo," alisema Hakimu Simba.

Alisema mahakama hiyo imejiridhisha kuwa mashtaka yote haijathibitisha isipokuwa shtaka la matumizi mabaya ya ofisi ya kuhamisha fedha kutoka akaunti ya Klabu ya Simba na kwenda akaunti binafsi.

Alisema kutokana na mashtaka hayo Nyange amekutwa hana hatia isipokuwa Aveva amekutwa na hatia ya kutumia nafasi yake vibaya kwa kuingiza fedha hizo kwenye akaunti binafsi ingawa hakuna wizi uliofanyika.

"Hela zote zilitumika kihalali isipokuwa tatizo lake hizo fedha ziliingizwa kwenye akaunti binafsi," alisema Simba.

Baada ya maelezo hayo Wakili wa Serikali Fatima Waziri alidai hawana kumbukumbu ya makosa ya jinai yaliyotendwa na mshtakiwa huyo hivyo naiomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe funzo kwake na kwa wengine wanaotumia madaraka vibaya ya ofisi.

Wakili wa utetezi Kuge Wabeya aliieleza mahakama hiyo kosa lake ni la kwanza, mshtakiwa ni mgonjwa amekutwa akihudhuria kliniki mara tatu kwa wiki na ana familia inayomtegemea.

"Tunaomba itoe adhabu nafuu itakayowezesha kuhudhuria kliniki na wakati akiwa anasubiriwa mshtakiwa alikaa mahabusu tangu mwaka 2017 hadi mwaka 2020," alidai Wabeya.

Hakimu Simba alisema kutokana na mazingira yaliyopo ya kesi amezingatia hoja za pande zote mbili kuwa mtuhumiwa amekaa mahabusu kwa muda mrefu.

"Kumpeleka gerezani kwa maana kumfunga haitasaidia chochote kwani watakuwa wamemfunga mgonjwa ambaye utakuwa umesababisha usumbufu siyo kwa mshtakiwa bali hata magereza na jamii kwa ujumla," alisema Simba.

"Hata ukimpiga faini kubwa bado haitasaidia chochote kwani asipolipa atalazimika kupelekwa gerezani hivyo adhabu pekee inayomfaa mahakama imeona atumikie kifungo cha nje miezi sita na asifanye kosa lolote," alisema.

Simba alisema rufani ipo wazi kwa yeyote ambaye hajaridhika na maamuzi hayo.

Katika kesi ya msingi ilidaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Kimarekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko Benki ya Barclays.



Rais wa Chama cha Wawekezaji Binafsi katika Elimu (TAPIE), Mahomoud Mringo (watatu kushoto), akizungumza baada ya kuchaguliwa kuongoza chama hicho kwa miaka mingine mitano kwenye mkutano mkuu, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni wanachama wa chama hicho. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Hoja tano za PAC kwa Jeshi la Polisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imetoa maagizo matano kwa Jeshi la Polisi ikiwamo kuchunguza na kuchukua hatua stahiki mara moja kwa waliobainika kufanya matumizi mabaya ya fedha ndani ya jeshi hilo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, aliyasema hayo jana baada ya kufanya mahojiano na jeshi hilo kuhusu hoja za ukaguzi za mwaka 2019/2020 kupitia fungu namba 28.

Alisema kuna fedha zimerejeshwa na wahusika (hakuweka wazi kiasi gani) na zilizobaki hakijarejeshwa ni zaidi ya Sh. milioni 419.

Alisema kuna baadhi ya fedha zimepelekwa kwenye jeshi hilo hazijatumika vizuri.

"Sasa uchunguzi umekuwa ukichukua muda mrefu sana na wakati mwingine ushahidi unakosekana kwa hiyo tumewagiza ofisa masuhuli ahakikishe wale wote wanaohusika wanachunguzwa na hatua stahiki zinachukuliwa mara moja bila kuchelewa," alisema.

Pia alisema kamati hiyo imeagiza majadiliano yaendelee kwenye miradi miwili ya nyumba wa uwekezaji wa Osterbay na Mtwara.

"Tumeagiza kuwa majadiliano yaendelee kufanyika kwasababu fedha nyingi zilikuwa zimeshatumika katika mradi huo ambao ni zaidi ya Dola za Marekani 827,000 zilikuwa zimeshatumika kwa hiyo tumesema mradi ule wa uwekezaji wa Osterbay uendelee wafanye majadiliano na wawekezaji kwa kuzingatia maslahi mapana ya taifa letu na taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kwa Katibu wa Bunge ifikapo Januari 7, mwaka 2022," alisema.

Alisema jambo jingine ni ujenzi wa miradi mbalimbali ya vituo vya polisi ambayo imesimama kwa muda mrefu kwa kukosa fedha na tatizo la kimkataba wameagiza ifanyike tathmini ili kujua fedha zinazotakiwa kukamilisha miradi yote.

"Kikijulikana kiwango cha fedha basi kipelekwe kwenye Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuiweka kwenye bajeti na fedha zitolewe," alisema.

Alitaja hoja nyingine ni kumekuwa na tatizo la utoaji wa mali na vidhibiti mbalimbali ambavyo vimekuwa vikichukuliwa na jeshi hilo.

"Unakuta kuwa kuna kesi nyingi zimekuwa zinapelekwa mahakamani mali zinabainisha na mahakama inatoa uamuzi baada ya kutoa uamuzi kunakuwa na changamoto ya utekelezaji wa maagizo hayo ya kimahakama baadhi ya vielelezo wale wanaoenda kutekeleza wanakuwa wako slow sana."

"Kwenye utekelezaji unakuta kama ni magari yalikamatwa yanatakiwa labda ya rejeshwe au yanatakiwa kuuzwa kama ni pikipiki zinatakiwa kuuzwa basi kumekuwa na ucheleweshaji sana wa utekelezaji wa maagizo hayo, kwa hiyo tumewagiza Katibu Mkuu ahakikishe mali zote zinazotolewa kama kielelezo pale ambnapo hukumu inakuwa imetolewa basi wahakikishe kwa kweli mali zote zinatolewa na utekelezaji wake unafamyika hilo nalo tumelitolea maaagizo," alisema.

Kuhusu madeni, aliagiza jeshi hilo kuweka mpango wa kulipa madeni ya wazabuni mbalimbali kiasi cha Sh. bilioni 631.4.

"Watengeneze mpango wa kuyalipa ili kuhakikisha wale wazabuni hawaathiriki kwa sababu kuna baadhi ya wazabuni watakuwa wametoa vifaa kwa jeshi hadi leo hawajalipwa unakuta mpaka mabenki wanaamua kuuza nyumba za wazabuni," alisema.

Kadhalika, aliagiza jeshi hilo kukusanya madeni ya Sh. bilioni 11 inayodai kwa watu mbalimbali zikiwamo faini za barabarani.

# Ujerumani yaipa Tanzania bil. 119.25/-

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI ya Shirikisho la Ujerumani imeipatia Tanzania msaada wa Sh. bilioni 119.25, kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji, afya, udhibiti wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na sekta ya utalii.

Mkataba wa fedha hizo ulifanyika jana jijini Dar es Salaam, Tanzania ikiwakilishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba na Serikali ya Ujerumani iliwakilishwa na balozi wake nchini, Regine Hess.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuingiwa kwa mikataba mitatu, Tutuba alisema kati ya fedha hizo Sh. bilioni 43.73 ni kwa ajili ya mradi wa kuboresha uhakika wa maji na udhibiti wa mabadiliko ya tabianchi na uboreshaji wa huduma za afya.

Alisema Sh. bilioni 22.53 ni kwa ajili ya mradi wa udhibiti wa magari ya kidigitali katika hifadhi za taifa ikiwamo Serengeti, Burigi-Chato, Katavi na Mikumi.

Tutuba alisema mkataba wa msaada uliosainiwa kati ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) wa Sh. bilioni 53, ni fedha za dharura kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa fedha uliotokana na ugonjwa wa virusi vya corona katika sekta ya maliasili.

Alisema mradi wa uboreshaji wa huduma za afya una malengo ya kuboresha kiasi na ubora wa huduma za afya kupitia bima ya afya katika Mikoa ya Tanga na Mbeya.

Tutuba alisema fedha hizo zitasaidia kupunguza vifo vya watoto wachanga, kinamama wakati wa kujifungua, pamoja na kuboresha mifumo ya TEHAMA ya hospitali.

Balozi wa Ujerumani, alisema ushirikiano wa nchi yake na Tanzania ulianza tangu mwaka 1961, kusaidia hifadhi za taifa na hifadhi za wanyama, ili kuongeza kipato.

Alisema maeneo mengine ni usafi, kuwasaidia Watanzania kupata majisafi, utawala bora na kusaidia wanawake na wasichana dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alisema fedha hizo zitakwenda kusaidia kufidia athari zilizotokana na ugonjwa virusi vya corona katika sekta ta utalii.

"Mapato katika sekta ya utalii wakati wa janga la corona yalishuka kutoka Sh. bilioni 2.6 hadi Sh. bilioni 0.75. Fedha tulizopokea leo zitakwenda kuwa mkombozi kwenye sekta ya utalii kwenye uhifadhi".

Dk. Ndumbaro alisema wizara inakwenda kufungua miundombinu katika hifadhi mpya, kuimarisha ujirani mwema, kupamba na kasi ya matukio ya ujangili kwa kutokomeza asilimia 10 iliyobakia.

## Flashi yaibua mvutano wa kisheria kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAWAKILI wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na wenzake, wamepinga kupokewa kwa video sita zilizoko kwenye flash kwa kuwa haikuonyeshwa mahakamani.

Pingamizi hilo liliwasilishwa jana na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda, wakati shahidi wa nane wa Jamhuri, Jonson Kisaka (35) wakati akitoa ushahidi. Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanakabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu.

Nyaraka nyingine zilizopingwa kupokewa mahakamani ni fomu namba 27, 28 na 29.

Akiwasilisha pingamizi hilo, Wakili Mahuna alidai kwamba vielelezo hivyo ikiwamo flashi, shahidi alifungua ripoti mwanzoni tu bila kucheza video sita zilizoko ndani yake.

"Tumepatiwa vielezo zikiwamo nyaraka na flash disk lakini shahidi amefungua ripoti hiyo ndani ya 'flash disk' na ameishia mwanzoni bila kufungua video sita zilizomo humo ndani kwa kuwa hatufahamu zinahusu nini," alidai Mahuna.

Pia alidai kwamba sheria inaelekeza wanapotoa vielelezo vinatakiwa kupitiwa kwa kufungua video hizo kutambua ni kitu gani kimeonyeshwa.

Alidai kwamba sheria imeelekeza na inataka kupatiwa kielelezo hicho kwa mapana yake ili kutambua ni kitu hani kimo ndani.

"Tunaomba mahakama isipokee kielelezo hiki na endapo itakipokea basi shahidi azungumzie sehemu za awali za mafaili ya video hizo na si kuzifungua na kuzungumzia," alidai Mahuna.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, alidai utaratibu wa kisheria umezingatiwa kwa kuwa shahidi ameonyesha vitu ambayo amevizungumzia wakati akitoa ushahidi wake.

Alidai kwamba Sheria ya Kielektroniki, kifungu cha 15, hakijaeleza kuwa kielelezo kinatakiwa kusomwa ndipo kipokewe mahakamani.

Naye Othmed Mtenga, Wakili Mwandamizi wa Serikali, aliiomba mahakama hiyo kupokea flash hiyo na nyaraka hizo kwa kuwa wamefuata utaratibu wa kisheria.

Alidai kwamba hoja hizo haizuii flash na nyaraka kupokewa kwa kuwa kinachoangaliwa ni kama shahidi anautambua ushahidi anaouzungumzia na kama amehusika kukiandaa. Pia alidai kisheria shahidi anatakiwa kuelezea kielelezo hicho kabla ya kukitoa mahakamani.

"Tunaiomba mahakama kupokea kielelezo hiki kwa kuwa shahidi ameeleza kwamba anakifahamu. Pia hoja ya kusema kielelezo kionyeshwe nini kilichomo ndani ni sawa na kukifungua kabla ya kupokewa kwanza kwa kuwa kiutaratibu kinatakiwa kupokewa ndipo kisomwe mahakamani.

"Tunaona hawajatoa hata sababu ya kisheria kupinga vielelezo hivyo na hawana muda tena wa kufanya hivyo, naona tayari wameshakubali vipokewe," aliodai Mtenga.

Baada ya hakimu kuzikiliza hoja za pande zote mbili, aliahirisha kesi hiyo Novemba Mosi, mwaka huu, majira ya saa 3:00 asubuhi.

TANGAZO

Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBER 2021.
Kiwango kwa Tzs.

| | | Robo Mwaka wa sasa 30-Sep-21 TZS | Robo Mwaka wa sasa 30-Jun-21 TZS |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 819,368,398 | 695,718,149 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 32,832,347 | 70,501,515 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 126,767,311 | 136,877,019 |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | | |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 14,544,415,369 | 15,130,080,151 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,535,111,154 | 1,400,823,903 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 | Akaunti za udhamini | | |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | **1,711,129,297** | **1,670,574,055** |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | 18,769,623,874 | **19,104,574,792** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 | Amana za Wateja | 2,154,646,532 | 1,356,985,905 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 | Amana Maalumu | 2,064,363,594 | 2,049,402,075 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | | |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | | |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi | | |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 229,836,593 | 277,251,945 |
| 28 | Madeni | 5,700,000,000 | 6,750,000,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **10,148,846,719** | **10,433,639,924** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **8,620,777,155** | **8,670,934,868** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 6,056,496,547 | 6,056,496,547 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | | |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | 2,439,473,000 | 2,439,473,000 |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | 56,434,051 | 107,960,208 |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | 68,373,556 | 67,005,113 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,620,777,155** | **8,670,934,867** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | | |
| 39 | Mikopo chechefu | 4,448,185,825 | 991,222,058 |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | 717,420,694 | 923,515,410 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | % | |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 45.93% | 45.00% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 30.58% | 6.55% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 362% | 471% |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 77% | 79% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81% | 84% |
| vi | Ongezeko la Amana | 1% | -7% |
| vii | Ongezeko la Mali | -2% | -2.00% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBER 2021
Kiwango kwa Tzs '(000)'

| | | Robo Mwaka wa sasa 30-Sep-21 TZS | Robo Mwaka wa sasa 30-Jun-21 TZS |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **56,434,051** | **107,960,208** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | | |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **100,702,752** | **97,720,253** |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | - | - |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | | |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | | **157,136,803** | **205,680,461** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | | |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | | |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 134,287,250 | (27,130,612) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 797,660,627 | (404,095,308) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 14,961,519 | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 47,415,352 | - |
| | | **1,151,461,552** | **(225,545,460)** |
| | - Kodi Iliyolipwa | (32,000,000) | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **1,119,461,552** | **(225,545,460)** |
| | | - | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (40,555,242) | - |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | Mengineyo Amana za kudumu | - | |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa*** | **(40,555,242)** | - |
| | | - | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | (955,619,586) | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (47,415,352) | 83,721,146 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | | |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **(1,003,034,938)** | **83,721,146** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha | **75,871,372** | **(141,824,314)** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | **903,096,683** | **1,044,920,997** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **978,968,055** | **903,096,683** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBER 2021

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa Hisa | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya juma | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Salio la wa mwaka 01/01/2020 | 6,056,497 | - | - | - | 69,693 | 2,332,349 | 8,458,539 |
| Rekebisho : | | | | | | - | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | - | - | (69,693) | - | (69,693) |
| Mapato mengine | | | | | | | - |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | | - | | 67,005 | - | 67,005 |
| Tozo la Mali la mwaka jana | - | - | - | - | - | 434,618 | 434,618 |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | (54,944) | (54,944) |
| Gawio lililolipwa | | | | | | (272,551) | (272,551) |
| **Salio kwa Mwaka 31.12.2020** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **67,005** | **2,439,472** | **8,562,974** |
| **Salio la mwaka 01.01.2021** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **67,005** | **2,439,472** | **8,562,974** |
| Rekebisho : | - | | | | | | - |
| Akaunti zingine za Mtaji | - | | | | 68,374 | (67,004) | 1,370 |
| Toa: Mapato mengine | - | | | | | | - |
| Mtaji wa kisheria | - | | - | - | | | - |
| | - | | | | | | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | | 56,434 | 56,434 |
| Toa: Gawio lililotolewa | - | | | | | - | - |
| **Salio kwa mwaka 31.09.2021** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **135,379** | **2,428,902** | **8,620,778** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBER 2021.
Kiwango kwa Tzs.

| | | wa sasa 30-Sep-21 TZS | wa sasa 30-Jun-21 TZS | wa sasa 30-Sep-21 TZS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,033,423,856 | 1,201,351,910 | 3,392,138,862 |
| 2 | Gharama za Riba | 150,931,913 | 104,475,324 | 349,611,013 |
| 3 | **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **882,491,943** | **1,096,876,586** | 3,042,527,849 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | -206,094,716 | 89,311,053 | -32,494,032 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **163,690,836** | **202,399,489** | 702,885,407 |
| | | 0 | | 0 |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 103,803,732 | 114,381,288 | 330,953,493 |
| | 6.3 Gawio | 0.00 | | |
| | 6.4 Mapato Mengine | 59,887,105 | 88,018,201 | 371,931,914 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,171,657,422** | **1,055,736,154** | 3,399,421,677 |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 618,195,313 | 627,391,742 | 1,879,093,222 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 13,035,652 | 348663.00 | 13,607,878 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 540,426,457 | 427,995,749 | 1,506,720,577 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **80,620,073** | **154,228,868** | 378,485,610 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 24,186,022 | 46,268,660 | 113,545,683 |
| 10 | **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **56,434,051** | **107,960,208** | 264,939,927 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | **0.00** | | |
| 12 | **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **56,434,051** | **107,960,208** | 264,939,927 |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 129 | 133 | 129 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 13 | 12 | 13 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 3 | 3 | 3 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 6% | 10.00% | 6% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 12% | 14.00% | 12% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 52% | 81.00% | 52% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6% | 9.00% | 6% |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2021

AINA YA BIDHAA

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | | 2. Mkopo | |
|---|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufungua akaunti | 5000/= | | Mikopo ya biashara | 36% PA |
| Ada ya mwezi | BURE | | Mikopo ya kuboresha nyumba | 18% PA |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | | Ada ya Mkopo | 2.50% |
| Kuuliza salio | BURE | | Bima ya mkopo | 2.00% |
| Kufunga akaunti | 5000/= | | Mikopo ya Jikimu | 17% PA |
| Gharama za kuendesha akaunti | 5000/= | | Mikopo ya Kilimo | 30% PA |
| Gharama za kuweka fedha | BURE | | Mikopo ya Maji | 26% PA |
| | | | Mikopo ya wafanyakazi | 15% PA |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| **Imesainiwa na:** | **Cheo** | | **Tarehe:** |
|---|---|---|---|
| *Altemius Millinga* | *Mkurugenzi Mtendaji* | .............................. | *28-Oct-21* |
| *Samwel Gikaro* | *Meneja wa Fedha* | .............................. | *28-Oct-21* |
| *Humphrey Singogo* | *Kaimu Mkaguzi wa Ndani* | .............................. | *28-Oct-21* |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| **Kuthibitishwa na:** | | | |
|---|---|---|---|
| *Ernest K. Ndimbo* | *Mwenyekiti wa Bodi* | .............................. | *28-Oct-21* |
| *Happy Sambega* | *Mkurugenzi* | .............................. | *28-Oct-21* |

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tujiandae mapema kukabili tishio ukame

**UTABIRI** wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) wa juzi hauhitaji muda wa kusubiri athari zitokee ndipo hatua zianze kuchukuliwa na mamlaka za serikali pamoja na wadau.

Utabiri huo ambao unaeleza kuwapo kwa upungufu wa mvua katika maeneo kadhaa ya nchi yetu wakati wa msimu wa vuli, unamaanisha kuwa kuna uwezekano wa kuwapo kwa athari mbalimbali, ukiwamo upungufu wa chakula.

Tunasema hivyo kutokana na mikoa maarufu ambayo huzalisha chakula kwa wingi hususan nafaka kuwa miongoni mwa mikoa ambayo itapata mvua za wastani au chini ya wastani.

Ikumbukwe kwamba mikoa hiyo mingi ikiwa ya Nyanda za Juu Kusini kuna wakati iliitwa kwa jina la 'The Big Four' kutokana na kuwa mzalishaji mkubwa wa nafaka hasa mahindi, hivyo kuwa tegemeo kubwa kwa uzalishaji nchini.

Katika taarifa yake ya utabiri juzi, TMA ilisema kwamba mikoa inayozalisha chakula kwa wingi nchini inatarajiwa kuwa na uhaba wa mvua na kwamba ni mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka kuanzia Novemba hadi Aprili mwakani.

Utabiri huo unaonyesha maeneo mengi ya mikoa yatakayopata mvua chini ya wastani na wastani kwa baadhi ya maeneo.

Mikoa hiyo inayotarajiwa kupata mvua pungufu ni Mbeya, Songwe, Ruvuma, Iringa, Rukwa, Katavi, Njombe, Lindi, Mtwara na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, alibainisha hayo mkoani Dar es Salaam na kufafanua kuwa hali hiyo inatokana na mifumo ya hali ya hewa, mvua za wastani mpaka chini ya wastani zinatarajiwa katika mikoa hiyo ikiwamo pia mikoa ya Kigoma, Tabora, Singida na Dodoma.

Kwamba hali ya sasa ya joto la bahari eneo la kati la Bahari ya Pacific iko chini ya wastani na inatarajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani katika nusu ya kwanza ya msimu. Alisema hii inatarajiwa kudhoofisha mifumo inayosababisha mvua katika maeneo ya pwani ya magharibi.

Alisema kutokana na hali hiyo inayotarajiwa kunaweza kutokea athari mbalimbali na kuwataka wananchi na mamlaka husika kuchukua tahadhari.

Katika sekta ya kilimo na usalama wa chakula kutokana na mvua za chini zinazotarajiwa, alisema kutakuwa na upungufu mkubwa wa unyevunyevu kwenye udongo na kuathiri ukuaji wa mazao, lakini kunatarajiwa kuwapo kwa visumbufu vya mazao kama mchwa, panya, viwavijeshi na wadudu wengine.

Aliwashauri wakulima kupanda mazao na mbegu zinazokomaa kwa muda mfupi na yanayostahimili mvua chache kama ya jamii ya mizizi na mazao ya bustani, akisema mazao haya ni kama mihogo, viazi, mtama na mazao mengine yenye kustahimili mvua chache.

Aidha, athari nyingine ni kwa upande wa mifugo na uvuvi ambapo kutokana na uhaba wa mvua hizo kunaweza kukaathiri upatikanaji wa samaki na uhaba wa malisho ya wanyama.

Kwa kifupi, sisi kama taifa tunapaswa kuanza kuchukua hatua za tahadhari kuanzia sasa, kwa kuwa ni dhahiri kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kutokea upungufu wa chakula.

Katika nchi zinazoendelea ambazo hazijawa na teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji, mvua inapokosekana maana yake ni ukame, hivyo ni dhahiri kwamba kutakuwa na upungufu wa chakula.

Tunaishauri serikali ianze maandalizi ya kusambaza chakula cha ziada katika maeneo yatakayokuwa na upungufu na kama ziada haitatosheleza, basi ikiagize kutoka nje. Kwa upande wao wakulima wapande mazao ya muda mfupi yanayostahimili ukame.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Ester Mgidula

# Jamani, baada kutunukiwa joho kipi kinafuata enyi wahitimu?

**WAHENGA** walinena; 'kurukaruka kwa maharagwe ndiyo kuiva kwake'. Ni msemo unaowaangukia wahitimu wa vyuo vikuu na wengine wanaofanana nao kielimu nchini.

Ni baada ya purukushani nyingi za namna tofauti kunoa ubongo wao kwa fani walizozipitia wakati wa 'kusotea' masomo yao, hatimaye wanahitimisha kwa kutunukiwa digrii ( kuvaa joho).

Utaratibu wa namna wanavyotunukiwa masomoni kuna ngazi zao za ufaulu zilizozoeleka kwa jina la ufupi 'G.P.A'. Ila wenyewe watunukiwa wana lugha yao ya masihara, lakini inamaanisha ya moyoni wakitamka, "kikubwa joho bwana, G.P.A inatafutwa mtaani."

Narudia tena inawezekana ikaishia hapo hapo kama msemo tu, ingawa kama inamaanisha au la bado ni kitendawili. Ni jambo la kufikiria kwa makini!

Zama za leo kimsingi zinatofautiana sana na hizo zilizopita.

Wenye zama hizo za kale kuhitimu ilikuwa kama kulima shamba na kupalilia, wakisubiri mavuno ya ajira kutoka mpango mkuu wa serikalini.

Leo hii kusubiri ajira ni sawa na kungoja kuwaona wazazi wako watakapokuwa vijana.

Haya yote yanatokana na sababu mbalimbali kama vile; kuongezeka kwa wasomi nchini na duniani, sayansi na teknolojia nayo inakua kwa kasi, kwahiyo zao lake nafasi za ajira zinabaki kuwa 'kiduchu', tukisikia hadithi ni sharti uwe na kinachoitwa mtaani 'connection'.

Lakini maisha lazima yaendelee wahitimu hamna budi kujiongeza kwa kujiajiri katika sekta mbalimbali, kama kilimo na biashara. Wapo wanaohoji mtaji je, watapata wapi ikiwa ndiyo wametoka vyuoni?

Jibu linaanzia kwa kufinya wazo, mtaji si lazima uanzie milioni, bali hata elfu kadhaa unazozimudu,unaumiza nazo kichwa. Bado nashikilia msimamo, fursa za kilimo na biashara bado ni kipande kipana kupindukia, muhimu ni mipango thabiti.

Tuanze na biashara; zipo kama za vyakula, vinywaji na nguo ndizo zinazofanyika kwa urahisi zaidi kwa sababu ni mahitaji ya msingi kwa binadamu, maana kula, kunywa na kuvaa hakukwepeki, kila siku iendayo kwa Mungu.

Kilimo je? Huenda wakazi wa mjini wakaguna, lakini ukweli kujikita katika mazao ya biashara yanalipa.

Hapo kuna mchele, mahindi, alizeti na kadhalika, yakifikia hatua bora ya mavuno na kuunganishwa kwa kusafirishwa kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi, wasomi mtajikuta katika uhusiano wa karibu na ajira, pia vipochi vyenu kutuna. Mpo wahitimu?

Najua shida yenu wasomi, mnajiegemeza sana viingereza, pia maisha ya kuigiza. Kumbukeni maisha ya nyumbani mlikotoka na namna ya kuwasaidia wazazi waliowasomesha hadi kuwafikisha hapo.

Acheni hayo majidai ya 'u-slay queen' na 'u-brother men'! Pigeni kazi yoyote, kama alivyotuasa Hayati JPM, sana sana kigezo na masharti kwenu iwe shughuli halali na isiyowaondolea utu.

Kwa sasa, jamii inahitaji nguvukazi kutoka kwenu vijana wasomi, tarajio la viongozi bora, washauri makini na werevu, mkiwa na imani tosha kutoka kwenye jamii iliyowasomesha hadi jirani kabisa na dari la elimu.

Ni zamu yao sasa kuchuma matunda kwenye miti yenu, ili mumuonyeshe Mama yenu, Mkuu wa nchi kwamba "kazi inaendelea" kwa manufaa ya jamii nzima na si kupotosha.

# Mwinyi: Idadi vifo vya Uviko haikuwa kubwa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa idadi ya vifo na maambukizi ya maradhi ya Uviko-19, kwa upande wa Zanzibar haikuwa kubwa kama ilivyotokea katika nchi mbalimbali duniani.

Hata hivyo, alisema athari za kiuchumi ni kubwa zaidi kuliko ilivyotokea katika baadhi ya nchi zilizokuwa na idadi kubwa ya vifo na maambukizi ya corona.

Aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya miaka 76 ya Umoja wa Mataifa ambayo yalifanyika mjini hapo. Alisema hali hiyo inatokana zaidi na utegemezi wa sekta ya utalii na za huduma kwa maendeleo ya uchumi wa nchi.

"Kuanguka kwa utalii kumeathiri sana kiwango cha ukusanyaji wa mapato, maendeleo ya biashara, usafiri wa anga na baharini, elimu, shughuli za ujasiriamali, ajira, kilimo, uvuvi na ufugaji, bila ya shaka, tukiwa na mifumo bora ya afya ndiyo msingi wa mapambano dhidi ya Uviko-19," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema kaulimbiu ya maadhimisho hayo isemayo 'kujijenga upya vizuri zaidi kwa kuweka mifumo bora ya afya' (Building back Better with Health System), imeweka msisitizo wa umuhimu wa kuwa na mifumo bora ya kiafya ili kupambana na maradhi ya Uviko-19 na kuishi katika hali ya usalama zaidi.

Pia, alisema kuna umuhimu wa kuwa na mifumo bora ya afya na kuongeza juhudi za kurejesha maisha katika hali yake ya kawaida kutaharakisha kasi ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika sekta zote za kiuchumi na kijamii.

Alisema kuwa maradhi ya corona, yamethibitisha umuhimu wa kuwapo Jumuiya za Kimataifa, kama Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ajili kuunganisha juhudi za mataifa na kupaza sauti katika kutoa miongozo na maelekezo muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Imani yake ni kwamba mataifa yote duniani yataongeza nguvu na kufanyakazi kwa pamoja ili kuhakikisha ushirikiano wa Umoja wa Mataifa na mashirika yake unazidi kuwa imara zaidi. Alisema Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano zitaendelea kutekeleza wajibu wao katika kuhakikisha umoja huu unakuwa imara na unafanya kazi kwa manufaa ya wanadamu na mataifa yote duniani.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema Umoja wa Mataifa ni chombo kilichoundwa kusaidia amani duniani na umoja huo una historia ndefu kuisaidia Tanzania ikiwamo katika mapambano ya corona.

Aliwataka wananchi kushirikiana kuchanja chanjo za corona ambazo zinatolewa bure ili kupunguza makali ya maambukizi ya ugonjwa huo pia kuchukua tahadhari za kujikinga.

Kwa upande wake Mratibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) Zanzibar, Zlatan Milisic, ameipongeza Zanzibar kuendelea kutekeleza malengo endelevu yaliyowekwa ikiwamo kupambana na athari za uharibifu wa mazingira na utunzaji wa fukwe licha ya kuwapo kwa tishio la mabadiliko ya tabia ya nchi. "Nimefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi ikiwamo kutunza mazingira hatua ambayo itasaidia juhudi za kutangaza utalii wa fukwe," alisema.

# Lori la TANESCO lanaswa tuhuma kusafirisha abiria

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeyakamata malori mawili, likiwamo la Shirika la Umeme (TANESCO), yakidaiwa kubeba shehena ya nguzo za umeme na vijana zaidi ya 20.

Kwa mujibu wa jeshi hilo, malori hayo yamekamatwa yakielekea vijijini kwenda kusambaza umeme, likidai kuwa kitendo hicho kinahatarisha maisha ya vijana hao.

Malori hayo yamekamatwa ikiwa ni siku chache baada ya lori lingine la TANESCO wilayani Mbarali mkoani hapa kupinduka katika eneo la Inyala, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kusababisha vifo vya vijana sita papo hapo.

Wakati wa kuaga miili ya vijana hao katika Uwanja wa Shule ya Msingi Igawilo jijini Mbeya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kuwakamata na kuwasweka ndani madereva wote wanaovunja sheria za usalama barabarani, wakiwamo wa serikali.

Homera alisema ajali zinazogharimu maisha ya watumishi wa umma mkoani humo zimeongezeka kutokana na madereva kuendesha vyombo hivyo bila kuchukua tahadhari na hivyo akasisitiza wakamatwe bila kujali anayemwendesha, hata kama ni mkuu wa mkoa huo. Akizungumza na wandishi wa habari katika Ofisi za Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani mkoani Mbeya, Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Ulrich Matei, alisema kukamatwa kwa malori hayo ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Homera.

Aliyataja malori yaliyokamatwa kuwa ni lenye namba za usajili SU. 37200 aina ya Mitsubish Truck, mali ya TANESCO, na lenye namba za usajili T. 923 DKC aina ya Mitsubish Fuso, mali ya Kampuni ya inayosambaza umeme vijijini mkoani Mbeya ya SAGCOM.

Alisema kwenye operesheni hiyo, waliwakamata madereva waliokuwa wanaendesha magari hayo ambao ni Mohamed Chongolo aliyekuwa anaendesha gari la TANESCO na Anthon Fungo aliyekuwa anaendesha gari ya mkandarasi.

"Ni hatari sana kubeba abiria kwenye magari ya mizigo, hawa madereva wataandika maelezo na tunawapeleka mahakamani.

"Kama mnakumbuka ni juzi tu watumishi sita wa TANESCO walifariki dunia kwenye ajali. Sasa hawa wanarudia yaleyale, tutaendelea kuwakamata," alionya Kamanda Matei. Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Meloe Buzema, alisema Sheria ya Usalama Barabarani kifungu namba 58 (II) kinakataza gari lolote la mizigo kupakia abiria na kwa yeyote anayekamatwa lazima achukuliwe hatua za kisheria.

Vilevile, alisema sheria hiyo inakataza mtu yeyote kukaa kwenye sehemu hatarishi anapokuwa amepanda chombo cha moto na hivyo madereva wa magari ya mizigo wanaopakia abiria wanakiuka sheria hiyo. Buzema alisema wataendelea kutoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa vyombo vyote vya moto pamoja na abiria ili kuhakikisha ajali za barabarani zinapungua katika mkoa huo. "Lengo letu ni kuhakikisha mkoa wetu unakuwa salama, maagizo tuliyopatiwa na mkuu wetu wa mkoa tutayasimamia na kuyatekeleza kwa nguvu zetu zote ili kuhakikisha mkoa wetu unakuwa salama," alisema Buzema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**
**"INSTITUTE OF CONSTRUCTION TECHNOLOGY (ICoT)"**

## TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'

**1. Utangulizi:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu katika Manispaa ya Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo / Changarawe kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi yaliyopangwa kufanyika kuanzia tarehe 15 Novemba hadi tarehe 10 Disemba 2021 kama ifuatavyo:-

| | Jina la kozi | Tarehe ya kuanza na kumaliza mafunzo | Mahali Mafunzo yatakapo fanyika |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 1 | Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana juu ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Nne (4)**<br>15/11/2021 – 10/12/2021 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. Masomo yatakayofundishwa: -**

(a) Kozi ya ukarabati na matengenezo ya Barabara za Udongo / Changarawe: Washiriki watajifunza mambo mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Pia, watajifunza mambo mbali mbali juu ya: mpango wa kazi (Planning), Uongozi sehemu za kazi na mbinu za usimamiaji wa kazi, vipimo vya kazi, usimamiaji wa mikataba, Uwekaji wa tabaka la changarawe pamoja na ujenzi wa makalavati. Kozi hii imekusudia kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kutosha katika kufanya na kusimamia kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe / udongo kwa ubora wa hali ya juu.

**3. Njia za ufundishaji**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo.

**4. Malengo ya kozi**
Masomo katika kozi hii yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara;
iv. Kwa wanakikundi, masomo haya yatawawezesha kusajili "Community Groups" kwa ajili ya kufanya kazi za ujenzi wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.Vikundi hivyo vikisajiliwa vitatambulika kisheria na vitaweza kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinayotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. Walengwa wa Mafunzo haya ni:-**
Vikundi vya wanawake na vijana (Community Based) wanaohitaji kujifunza kazi za barabara.

**6. Lugha ya mafunzo:-**
Lugha itakayo tumika kufundishia katika kozi hii ni Kiswahili na kiingereza.

**7. Gharama za Mafunzo:-**
Gharama za mafunzo ni shilingi za Tanzania laki tano (500,000.00) ambazo zitagharamia chakula, malazi pamoja na vifaa vya kuandikia.

Ada ya ushiriki ilipwe kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki moja kabla ya kozi kuanza.

**8. Namna ya Kutuma Maombi ya Kozi hizi:-**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi hii wanatakiwa kutuma maombi yao Chuoni ICoT, tawi la Mbeya kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**Wasiliana nasi**

**Mkuu wa Chuo**
**IcoT- Mbeya**
**Wilaya ya Rungwe**
**S.L.P 1957, MBEYA,**

**Simu : 025 295 7484/5; 0787 059 555; 0769 317 404; 0765 251 509**
**Nukushi : 025 295 7486**
**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com**


**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com**

# Mipango miji watakiwa kutenga maeneo ya biashara za kawaida

**Na Munir Shemweta,**
MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka wataalamu wa mipango miji kuhakikisha wanapopanga mipango yao kwenye maeneo mbalimbali, wanatenga maeneo ya wafanyabiashara wa kawaida ili kufanya biashara katika mazingira rafiki na yaliyo bora.

Akizungumza wakati wa kufunga Mkutano Mkuu wa Saba wa Wataalamu wa Mipangomiji juzi mjini hapa, Dk. Mabula alisema mipango ya uendelezaji miji na michoro ya mipangomiji inapoandaliwa, ipelekwe mitaani katika lugha ambayo wana mitaa wanaweza kuielewa.

Baada ya wataalamu hao kutekeleza wajibu wao wa kupanga, halmashauri ambazo ni mamlaka za upangaji ziweke miundombinu ili wafanyabiashara hao wapatikane kwenye maeneo maalum yaliyotengwa.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, maeneo yatakayotengwa kwa ajili ya wafanyabiashara wa kawaida ni sharti yawe na huduma zote muhimu kama vile maji, umeme na barabara ili kuwawezesha kufanya biashara hata usiku.

"Mnapoandaa michoro yenu ya mipango miji zingatieni taaluma huku mkikumbuka kuna makundi maalum kama vile mamalishe, machinga, bodaboda na Watanzania wa kawaida na muwawekee utaratibu maalum wa kupata ardhi kwa gharama nafuu ili nao washiriki kujenga maeneo yaliyopangwa," alisema.

"Mipango ya uendelezaji miji inapoandaliwa iletwe mitaani katika lugha ambayo wana mitaa wanaweza kuielewa ili wasimamie kwa sababu wao ndio wadau na watasaidia hata katika udhibiti wa maendeleo," aliongeza.

Pia aliwataka wataalamu wa mipangomiji kushirikisha watendaji kata, mitaa na vijiji katika mipango ya uendelezaji mji kwa kuwa wao ndio wadau muhimu na kusisitiza kuwa wadau hao ni nguvu kazi itakayosaidia kupunguza ujenzi holela kwenye maeneo ya mijini na vijijini.

Naibu Waziri aliwataka wataalamu wa mipangomiji kuwa wabunifu na kuandaa miradi shirikishi isiyo na fidia na kubainisha kuwa miradi hiyo ni lazima itafanikiwa kwa kuwa itakuwa imeshirikisha wananchi watakaojiona kama sehemu ya wamiliki wa miradi hiyo.

Pia aliitaka Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipangomiji kuendelea kusimamia nidhamu, maadili na uwajibikaji kwa wataalamu wa sekta hiyo ili kuleta ufanisi katika sekta ya mipangomiji.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipangomiji, Prof. Wilbard Kombe, alimweleza Naibu Waziri kuwa katika maazimio yao wajumbe wa mkutano huo walipendekeza kufanyika mabadiliko kwenye sheria Na. 4 kwenye kifungu kinachohusu mfuko wa fidia ili watumiaji wakubwa wa ardhi wachangie mfuko huo.

"Tumeona huu ni wakati mwafaka kwa watumiaji wakubwa wakachangia katika huu mfuko ili kuipa nguvu wizara kumudu gharama zinazotokana na fidia hasa baada ya ardhi kuwa na thamani, kutegemea wizara moja kumudu jukumu hili ni ngumu sana, hivyo tumeona ni wakati muafaka kufanya mabadiliko kwenye sheria hiyo," alisema Kombe.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Total Energies Marketing Tanzania Ltd, Jean Francois Schoepp (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa tatu wa shindano la kuwawezesha wajasiriamali wachanga la Startupper of the Year Challenge kwa mwaka 2021-2022, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja Mawasiliano wa kampuni hiyo, Jaila Tindwa na Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano, Getrude Mpangile. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Upanuzi wa kiwanda kuongeza tani 144,000

**Na Mwandishi Maalumu,**
MOROGORO

UPANUZI wa kiwanda cha sukari cha Kilombero unatarajia kuongeza upatikanaji wa sukari kwa kuzalisha tani 144,000 za ziada kwa mwaka kulinganisha na kiwango cha sasa.

Hatua hiyo ya upanuzi wa kiwanda inatokana na serikali kushirikiana na kampuni ya Sukari ya Kilombero, ili kuongeza uwezo wa kuzalisha bidhaa hiyo muhimu kwa matumizi ya nyumbani na viwandani.

Mradi huo wenye gharama ya Sh. bilioni 584 ulioanza kutekelezwa Mei, mwaka huu, unatarajiwa kukamilika Juni, 2024 na kuwezesha kiwanda hicho kufikisha tani 271,000 kwa mwaka. Kwa sasa kiwanda hicho kinazalisha tani 127,000 kwa mwaka.

Akizungumza kuhusu mradi huo aliopotembelea kiwandani hapo juzi, Msajili wa Hazina, Mgonya Benedictom aliagiza kasi na ufanisi katika utekelezaji wake, ili kufanikisha juhudi za serikali za kuondoa uhaba wa sukari nchini.

Pia alisema mradi huo unatarajia kuongeza pato la serikali pamoja na kutoa ajira kwa wananchi wanaozunguka mradi huo.

# NMB yapata faida ya bil. 211/- baada ya kodi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA robo ya tatu ya mwaka iliyoishia Septemba 2021, Benki ya NMB imeonyesha ufanisi mkubwa na mafanikio katika maeneo mbalimbali ya kimkakati na kupata faida ya Sh. bilioni 211 baada ya kodi.

Imesema asi ya ongezeko la mapato iliendelea huku uwekezaji katika maeneo mapya na utekelezaji mipango endelevu ya kidijitali nayo ikiimarishwa pia.

Matokeo ya kuimarika kiutendaji yameiwezesha NMB kupata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 302 na faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 211, hili ni ongezeko la asilimia 43 ya faida iliyopatikana kipindi kama hicho mwaka jana na zaidi ya faida ya mwaka wote wa 2020 ambayo ilikuwa ni Sh. bilioni 206.

Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna, alisema jana kuwa nidhamu ya hali ya juu ya NMB katika kutekeleza mipango yake ya kimkakati imeendelea kuiongezea imani kwa wateja na hivyo na kuifanya iimarike zaidi kwenye nafasi yake ya benki inayoongoza nchini.

Katika kipindi cha miezi 9 kufikia mwezi Septemba 2021, jumla ya mapato ya NMB yalikuwa ni Sh. bilioni 721, kiasi ambacho ni asilimia 20 zaidi ya Sh. bilioni 601 zilizopatikana kipindi kama hicho mwaka 2020 ikichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mikopo na miamala.

Alisema mikakati ya benki ya kudhibiti gharama za uendeshaji imeendelea kuzaa matunda na kusababisha kuboreka kwa uwiano wa matumizi na mapato halisi kufikia asilimia 47 kutoka asilimia 52, kiwango kilicho ndani ya matakwa ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) cha asilimia 55. Benki inaendelea kuboresha utendaji kazi na uwekezaji hasa kwenye maeneo ya kimkakati.

Alisema ubora wa mikopo umeendelea kuimarika ambapo uwiano wa mikopo chechefu umeshuka hadi asilimia 3.8 kwenye robo ya tatu, kutoka asilimia 6.6 kipindi kama hiki mwaka jana ikionyesha hatua nzuri iliyopigwa kudhibiti ukopeshaji usiokuwa na tija.

"NMB imeendelea kuwa na mizania madhubuti ambayo ukuaji wake unaonyesha kuimarika kwa mahusiano na wateja wetu. Mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka, mikopo iliongezeka kwa asilimia 13 hadi kufikia shilingi trilioni 4.5 kutokana na kukua kwa mikopo kwenye maeneo muhimu hasa kilimo, biashara ndogo na za kati pamoja na mikopo binafsi," alisema Zaipuna.

Alisema amana za wateja nazo ziliongezeka kwa asilimia 18 mpaka shilingi trilioni 6.1 kufikia Septemba 30, 2021 ukilinganisha na shilingi trilioni 5.3 Septemba 2020 kutokana na NMB kuendelea kutoa suluhisho stahiki katika kuimarisha urahisi na upatikanaji wa huduma za kibenki kwa wateja.

Kwa mujibu wa Zaipuna, mali zote za benki zilikuwa na thamani ya shilingi trilioni 8.2 mwishoni mwa Septemba 2021, ongezeko la asilimia 17 (YoY) kutoka TZS trilioni 7 kipindi kama hicho mwaka jana.

## Nchi za Kiislamu zatangaza Wiki ya Umoja wa Kiislamu

**Na Kulwa Mzee**

MKURUGENZI wa Kituo cha Utamaduni cha Iran, Morteza Pirani, amesema Oktoba 19 hadi 24 kila mwaka zimetangazwa rasmi kuwa Wiki ya Umoja wa Kiislamu ulimwenguni.

Pirani alisema wiki hiyo muhimu ilimalizika Oktoba 24, mwaka huu.

"Nchi za kiislamu zina mambo mengi yanayofanana na yanayozipa uwezo wa kuimarisha umoja na mshikamano wao.

"Mbali na suala la uislamu nchi hizo zina mambo mengine mengi yanayofanana zikiwamo lugha ambazo zinaweza kuzifanya kuwa kitu kimoja, zinafanana kiutamaduni, kisiasa na kijamii na kwa kawaida zinapaswa kuwa na uhusiano mzuri," alisema.

Alisema umoja unaohitajika hauonekani popote kati ya nchi hizo jambo linaloibua swali kwamba ni kwa nini kuna hitilafu na uhusiano mbaya kati ya nchi za Kiislamu licha ya kuwapo mambo hayo yote yanayopaswa kuziweka pamoja.

Alisema katika uwanja wa ndani kuna baadhi ya mambo ambayo yanazua hitilafu kati ya nchi za Kiislamu huku akitolea mfano katika baadhi ya nchi kuna vitu vinavyoibua hitilafu na kutumiwa vibaya na maadui kwa ajili ya kufikia malengo yao dhidi ya uislamu katika nchi hizo.

"Siasa za madola makubwa ndiyo sababu kuu inayozuia nchi za Kiislamu kuwa na umoja, baadhi ya mivutano ya ndani ambayo inaonekana katika nchi za Kiislamu pia inatokana na siasa za kikoloni zilizotekelezwa katika nchi hizo katika karne zilizopita na madola ya Magharibi na hasa Uingereza.

"Kuibua na kuchochea mambo kama hitilafu za Shia na Suni, Waarabu na Waajemi, Waarabu na Wakurdi, Wafursi na Waturuki au Waarabu na Waturuki hayo yote ni katika mbinu na siasa zinazotumiwa na madola ya kikoloni ya Magharibi kwa ajili ya kuibua hitilafu na mifarakano kati ya nchi za Kiislamu.

"Suala lingine muhimu ni kwamba umoja na mshikamano wa nchi za Kiislamu unahatarisha maslahi na usalama wa utawala wa Israel," alisema.

Alisema kwa kutilia maanani ukweli huo wanasema sababu za nje zinazotokana na siasa za madola makubwa ya Magharibi ndiyo kizuizi kikuu katika njia ya kupatikana umoja wa nchi za Kiislamu.

Aliongeza kuwa madola ya kibeberu ya Magharibi yameamua kusimama imara kwa ajili ya kukabiliana kwa kila mbinu na juhudi zozote za kupatikana umoja na mshikamano katika nchi za Kiislamu.

# Makalla awaondoa hofu w/biashara wa Kariakoo

**Na Christina Mwakangale**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewaondoa hofu wafanyabiashara wa soko dogo Kariakoo maarufu soko la mabati, kwamba kuondolewa kwao eneo hilo ni kwa ajili ya kufanya ukarabati pamoja na ujenzi.

Amesema ni kuboresha mazingira ya kufanyia biashara.

Alisema juzi kuwa wafanyabiashara hao wanatambuliwa na hawamo kwenye orodha ya makundi matano yanayohamishwa ikiwamo wanaofanyia biashara maeneo yasiyo rasmi.

Makalla aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe, kujibu suala la wafanyabiashara wa soko hilo ambao juzi wakidai wanahamishwa eneo hilo bila kupewa taarifa za awali.

"Wafanyabiashara wa soko dogo hawako katika makundi matano yanayotakiwa kuhama. Siyo walioopo kwenye 'road reserve' (hifadhi ya barabara), mitaro, njia ya wapita kwa miguu, mbele ya maduka wala kwenye taasisi za umma.

"Hawahamishwi kama wamachinga ila watahamishwa kupisha ujenzi wa soko kwa faida yao wao," alisema Makalla.

Juzi, wafanyabiashara wa soko dogo la Kariakoo takribani 1,000 wakizungumza na waandishi wa habari, walidai kwamba, uongozi wa mkoa umewapa muda mfupi kabla ya kuondolewa eneo hilo, wakidai siku 10 walizopewa, hazitoshi.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Soko dogo la Kariakoo Dar es Salaam, Hussein Magae, alisema wameshangazwa na uamuzi wa kwamba waondoke eneo hilo haraka, bila kuzingatiwa idadi yao, akisema wapo sokoni hapo kisheria.

Magae aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari sokoni hapo, kuhusu kutakiwa kupisha ujenzi wa jengo la ghorofa nane.

Alisema wakiwa kama wadau wa maendeleo na wanaofanya biashara kwenye eneo lililothibitishwa kisheria ikiwamo kulipa kodi, ni vyema washirikishwe katika kila hatua ya kuendeleza soko hilo.

"Kuna taarifa kwamba soko hili dogo kunatakiwa kujengwa jengo la ghorofa la nane. Tuko zaidi ya 1,000 iweje tupewe siku chache," alisema Magae.

Mmoja wa wafanyabiashara katika soko hilo, Arcardo John alisema ni kawaida yanapofanyika mabadiliko hutolewa taarifa mapema na kwamba wanafanya biashara eneo hilo kwa mujibu wa sheria kutokana na kulipa kodi.




Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara kwa Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (wanne kushoto) pamoja na mmoja wa mteja wa benki hiyo, Scholastica Ponela (watatu kulia), wakibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi wa kadi mpya za benki hiyo zinazofahamika kama 'NBC Visa Debit Card' ikiwa na mwonekano wa wima wakati wa uzinduzi huo jijini Dar es Salaam juzi. Mwingine ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Benki Kidijitali, Deogratius Mosha (watatu kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# Muamala sasa hadi mil. 40/- NBC mara moja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imezindua kadi mpya 'NBC Visa Debit Card' yenye kuwawezesha wateja binafsi kufanya miamala inayofikia hadi Sh. milioni 40 kwa mara moja ilihali wateja wa kawaida wakifanya miamala inayofikia milioni 10 kwa mara moja.

Akizindua kadi hiyo mpya ya kidijitali ikiwa na mwonekano wa wima, Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara kwa Wateja Binafsi Benki ya NBC, Elibariki Masuke, alisema kadi hiyo inaiwezesha NBC kuunganisha mifumo yake mbalimbali ya malipo kwa njia tofauti mbalimbali.

"Tunazindua kadi yetu yenye nembo maarufu ya Twiga inayotambulisha Benki ya NBC. Kadi hii ina teknolojia ya NFC yaani tap and go.

"Kwa kutumia teknolojia iliyopo kwenye kadi hii, itatupatia uwezo wa kufanya malipo katika sehemu ambazo benki inatoa huduma kama vile viwanja vya michezo, usafiri wa umma ambao ni treni, magari ya mwendokasi na sehemu nyingine," alisema.

Masuke alisema ni salama kwa matumizi kwani imethibitishwa na VISA International hatua ambayo inaiwezeshwa kufanikisha miamala ya ndani na nje ya nchi.

Pia kadi hiyo ina uwezo wa kudumu kwa muda wa miaka mitano bila kuharibika.

Alisema kadi hiyo inatolewa kwa wateja wapya pindi wanapofungua akaunti na wale wenye akaunti ndani ya NBC wanaweza kwenda kwenye matawi ya benki hiyo na kupatiwa kadi hizo.

"Ni kadi bora kwani inapopita kwenye mashine za ATM haina mkwamo-mkwamo," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha huduma za Benki Kidijitali -NBC, Deogratius Mosha, alisema uzinduzi wa kadi hiyo unatokana na matunda ya ubunifu wa kazi zinazofanywa na benki hiyo.

"Kwa miaka 10 Benki ya NBC imekuwa ikiwekeza katika mifumo ya kiteknolojia na rasilimali watu ili kuhakikisha benki inakuwa namba moja katika utoaji wa huduma za benki kidijitali hapa nchini.

"Tumejikita katika uundaji wa mifumo mbadala, kuwezesha wateja wetu kupata huduma za benki popote walipo bila kufika katika matawi ya benki," alisema.

Alisema mifumo hiyo inajumuisha huduma zinazopatikana katika mashine za ATM, ambazo ni utoaji wa huduma za kibenki kwa njia ya simu, miamala ya kibenki na huduma nyingine.

"Pia kuna dawati maalumu la ubunifu ambalo linasimamia ubunifu wa bidhaa na mifumo inayolenga kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za kibenki pamoja na kuboresha huduma kwa wateja waliopo hapa nchini na wale waliopo nje ya nchi," alisema.

Aidha, alisema Benki hiyo itaendelea kuwekeza katika ubunifu wenye tija na kutoa huduma ambazo zinakidhi matakwa kwa wateja wa benki hiyo.

# Adaiwa kujinyonga kisa ugumu wa maisha

**Halima Ikunji,** TABORA

MICHAEL Paul (18), mkazi wa Lwanzali mkoani Tabora, anadaiwa kujinyonga kwa kutumia shuka chumbani kwake na kuacha ujumbe kwamba amefanya hivyo kutokana na ugumu wa maisha.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani Tabora, Richard Abwalo, alisema kuwa Oktoba 24, mwaka huu, majira ya saa saba usiku, katika Manispaa ya Tabora, kijana huyo alijinyonga kwa kutumia shuka lake.

Kamanda Abwalo alisema taarifa ya tukio hilo ililipotiwa kituo cha polisi na dada wa marehemu, Jane Paul, na kwamba kabla ya kifo chake, kijana huyo aliacha ujumbe wa maandishi.

Abwalo alisema ujumbe ulioachwa na kijana huyo, ulisomeka 'mama naomba unisamehe, ni maisha tu ndio yamenifanya nijiue, naomba mnizike'.

Kamanda huyo alisema chanzo cha kujinyonga ni msongo wa mawazo na mbinu alioitumia ni kujifungia ndani ya chumba kisha kujitundika na kupoteza maisha.

Marehemu huyo alijitundika kwenye kenchi kwa kutumia shuka yake katika chumba ambacho alikuwa analala na mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani Kitete mkoani Tabora.

Kamanda Abwalo alisema mwili huo umehifadhiwa kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu katika hospitali hiyo.

Alisema mtu akikutana na shida mbalimbali, anapaswa kushirikisha viongozi wa dini pamoja na jamii kutoa taarifa ya vituo vya polisi inapoona kuna viashiria vyote vya uvunjifu wa amani.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Deograsia Liganga (kushoto), akitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wanaotoka katika mazingira magumu wanaosaidiwa na Mradi wa Youth Agency Mufindi na Foxes Community and Wildlife Trust wilayani humo jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# BAKITA yaita wakalimani lugha za alama

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Kiswahili la Taifa (BAKITA), limeanza kutekeleza kwa vitendo agizo la serikali la kubaini wakalimani wa lugha ya alama ili kuondoa ombwe kubwa la kimawasiliano lililopo kwa sasa.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Lugha kutoka Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Mnata Resani, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Saalam wakati wa uzinduzi wa kuwabaini wakalimani wa lugha za alama ambao watatunzwa katika kanzidata ya BAKITA kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi.

Dk. Resani alisema kwa sasa Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) inahitajika kutokana na mahitaji kuwa makubwa.

"Mahitaji yanakwenda sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia, yatavihitaji vyombo vya habari, asasi za kiserikali na za kibinafsi zinazotoa huduma kwa umma pamoja na taasisi za elimu kuwa na wakalimani wa lugha ya alama ili kuondoa ombwe kubwa la kimawasiliano lililoko kwa sasa," alisema.

Pia alisema serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, wizara, asasi za umma na binafsi, wamejipanga kutekeleza kikamilifu malengo ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa 2020.

"Tunaliagiza BAKITA kwa kushirikiana na wadau wengine kuwaandaa wakalimani wa lugha ya alama wa kutosha ili nchi iwe na uwezo wa kuwapata kwa urahisi kwa ajili ya kutoa huduma katika sekta muhimu na mikutano ya kitaifa na kimataifa," alisema.

Dk. Resani aliwataka Watanzania wenye utaalamu wa ukalimani wa lugha ya alama ya Tanzania na wanaojua ukalimani wa lugha za alama za kimataifa kama vile Kiingereza, Kireno, Kichina, Kifaransa, Kijerumani, Kiarabu waende BAKITA kupata usajili na mafunzo.

"Wataalamu wengine wa ukalimani wa lugha ya alama kama vile walimu na wanaotoa huduma hii waje wasajili katika kanzidata ya BAKITA haraka iwezekanavyo, hii ni kwa sababu tumeweka utaratibu vizuri wa kuwawezesha Watanzania wenye taaluma hii kupata fursa za ukalimani zinazojitokeza ndani ya nchi," alisema.

Kaimu Katibu Mtendaji wa BAKITA, Consolata Mushi, alisema uzinduzi huo umefanyika kutokana na maelekezo ya serikali kwa baraza hilo yaliyowataka kuandaa kanzidata ya wataalamu wa ukalimani wa lugha ya alama ambao itawatumia kulingana na uhitaji.

"Mchakato huu umehusisha vyama maalum vitakavyojihusisha na watu wenye ulemavu kama vile Chama cha Wakalimani wa Lugha ya Alama Tanzania (CHAWALATA), Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) na wadau wengine," alisema.

Alisema mchakato huo ni endelevu na BAKITA limejipanga kuwafikia wakalimani ili liwasajili na kuwaingiza kwenye kanzidata ya baraza.

"Kuwapo kwa kanzidata rasmi ya wakalimani wa lugha ya alama kutaleta mafanikio hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa linajihusisha na utatuzi wa matatizo mbalimbali yanayogusa jamii hasa ya watu wenye ulemavu," alisema.

Consolata alisema matatizo wanayaona kwa sasa ni baadhi ya vyombo vya habari, asasi za serikali na binafsi zinazotoa huduma kwa jamii na usuluhishi wa migogoro kutokuwa na wakalimani maalum wa lugha ya alama.

Awali, Mwenyekiti wa CHAWALATA, Suzan Mtui, aliomba serikali iwafikie wakalimani walipo mikoa mbalimbali ambao nao wana uwezo tofauti tofauti.

Pia aliomba BAKITA, CHAVITA na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na wakufunzi kutoka CHAWALATA kuandaa mpango wa kuwatumia katika kufundisha wakalimani wapya.

## Akutwa na kesi ya kujibu kwa mauaji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imemuona mkazi wa Kijiji cha Ngura, Kata ya Bujura Wilaya Geita, Manoni Isheli ana kesi ya kujibu baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wao.

Isheli ameshtakiwa kwa kosa la kumuua kwa makusudi mama yake mzazi Njombile Manoni (90) kwa kumcharanga kwa mapanga kichwani na kufariki dunia papo hapo.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana Mbele ya Jaji wa Mahakama hiyo, Fredrick Manyanda na aliposomewa shtaka lake alikana kuhusika na kosa hilo.

Manyanda alisema upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alipeleka mahakamani mashahidi wawili pamoja na vielelezo viwili ambavyo vilionyesha kuwa mshtakiwa huyo ana kesi ya kujibu na mahakama hiyo kumtaka ajitetee.

Aidha, Jaji Manyanda aliuliza upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili wa Kujitegemea, Penina Mashimba, kuwa mteja wake atajitetea kwa namna gani, Mashimba alidai mteja wake atajitetea kwa kiapo na atajitetea peke yake bila kielelezo wala shahidi mwingine.

Jaji Manyanda aliahirisha kesi hiyo hadi leo kwa ajili ya mshtakiwa huyo kutoa utetezi wake baada ya kukutwa na kesi ya kujibu.

Awali akisoma hati ya mashtaka Karani wa Mahakama hiyo, Felister Mlolwa, alidai kuwa Oktoba 14, 2015 majira ya mchana mshtakiwa alimuua mama yake mzazi Njombile Manoni kwa kukusudia kwa kumcharanga kwa mapanga kichwani na kufariki dunia.

**Aidha, Jaji Manyanda aliuliza upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili wa Kujitegemea, Penina Mashimba, kuwa mteja wake atajitetea kwa namna gani, Mashimba alidai mteja wake atajitetea kwa kiapo na atajitetea peke yake bila kielelezo wala shahidi mwingine.**

TANGAZO

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## Tanzu ya Citigroup, Kampuni iliyoshirikishwa nchini Marekani

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-21 |
|---|---|---|
| **A . MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 18,216 | 8,434 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 60,230 | 70,185 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 174,530 | 175,478 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 154,758 | 92,834 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 173 | 105 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | 13,557 | 13,419 |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 27,068 | 36,245 |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 168,261 | 192,471 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 308,465 | 299,869 |
| 12 Mali Nyingine | 10,550 | 9,528 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 7,799 | 8,022 |
| 16 **JUMLA YA MALI** | **943,607** | **906,590** |
| **B . DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 785 | 517 |
| 18 Amana za Wateja | 619,328 | 735,670 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 Amana Maalumu | 9 | 613 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,489 | 2,394 |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,042 | 2,062 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 27,071 | 36,248 |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 736 | 660 |
| 27 Dhima Nyingine | 26,999 | 25,833 |
| 28 Madeni | 161,553 | 5,000 |
| 29 **JUMLA YA DHIMA** | **842,012** | **808,997** |
| 30 **MALI/(DHIMA) HALISI** | **101,595** | **97,593** |
| **C . FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 - Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,660 | 9,660 |
| 32 - Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 - Mapato Yaliyobakizwa | 81,553 | 82,125 |
| 34 - Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 6,878 | 3,790 |
| 35 - Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,504 | 2,018 |
| 36 - Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| 37 **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **101,595** | **97,593** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 60,835 | 107,300 |
| 39 Mikopo Chechefu | 0 | 0 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 968 | 883 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| **D . BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| ( i ) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.8% | 10.8% |
| ( ii ) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.0% | 0.0% |
| ( iii ) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 49.7% | 40.7% |
| ( iv ) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 32.7% | 33.1% |
| ( v ) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 67.6% | 62.7% |
| ( vi ) Ongezeko la Amana | -18.8% | -17.8% |
| ( vii ) Ongezeko la Mali | 3.9% | -15.4% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 7,937 | 7,311 | 23,152 | 24,517 |
| 2 Gharama za Riba | (1,226) | (3,692) | (5,833) | (9,828) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba** | **6,711** | **3,619** | **17,319** | **14,689** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (86) | 135 | (319) | (467) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **3,656** | **3,272** | **10,276** | **9,514** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 2,357 | 2,216 | 6,470 | 6,040 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,300 | 1,056 | 3,807 | 3,474 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | (1) | 0 | (1) | 0 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,984)** | **(5,875)** | **(17,457)** | **(18,718)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,227) | (1,688) | (6,714) | (5,646) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (3,757) | (4,187) | (10,743) | (13,072) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **4,297** | **1,151** | **9,819** | **5,018** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (1,210) | (337) | (2,942) | (2,447) |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **3,088** | **814** | **6,878** | **2,571** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | |
| Mapato ambayo hayajakamilika | 1,306 | (563) | 1,224 | (120) |
| Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | (392) | 169 | (367) | 36 |
| Mapato mengine baada ya kodi ya mapato | 914 | (394) | 857 | (84) |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | **4,002** | **420** | **7,735** | **2,487** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 47 | 44 | 47 | 44 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 308,755 | 81,435 | 687,761 | 257,070 |
| 15 Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **D . BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| ( i ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.4% | 0.2% | 0.9% | 0.3% |
| ( ii ) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 12.3% | 3.4% | 9.3% | 3.5% |
| ( iii ) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 57.7% | 85.3% | 63.3% | 77.3% |
| ( iv ) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 4.4% | 3.1% | 3.2% | 4.1% |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Imesainiwa na: Geofrey Mchangila (Ofisa Mtendaji Mkuu) Date : 28 Octoba 2021

Imesainiwa na: Iddi Msonga (Mkuu wa Fedha) Date : 28 Octoba 2021

Imesainiwa na: Godwin Rutashobya (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) Date : 28 Octoba 2021

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

Imesainiwa na: Andulile Mwakalyeye Date : 28 Octoba 2021

Imesainiwa na: Yande Panya Date : 28 Octoba 2021

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-21 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 4,297 | 3,111 | 9,819 | 5,018 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| -Hasara Katika Mali | 536 | 448 | 1,429 | 1,501 |
| -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (8,595) | (1,510) | 1,948 | (26,369) |
| -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 1 | 0 | 1 | 0 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (116,074) | (130,805) | (547,975) | 866,128 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | 0 | 0 | 0 | 0 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (7,809) | 8,798 | (12,916) | 9,835 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 7,349 | (10,673) | 4,824 | (13,114) |
| -Kodi Iliyolipwa | (605) | (689) | (1,899) | (2,703) |
| -Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(120,900)** | **(131,320)** | **(544,769)** | **840,296** |
| **II . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (298) | (18) | (350) | (2,761) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 2,254 | (1,930) | (22,856) | 31,680 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **1,956** | **(1,948)** | **(23,206)** | **28,919** |
| **III . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 156,553 | (20,000) | 161,553 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **156,553** | **(20,000)** | **161,553** | **0** |
| | **37,609** | **(153,268)** | **(406,422)** | **869,215** |
| **IV . Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **37,609** | **(153,268)** | **(406,422)** | **869,215** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 364,029 | 517,297 | 808,060 | 378,979 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 401,638 | 364,029 | 401,638 | 1,248,194 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | **0** | **85,916** | **1,582** | **0** | **1,759** | **98,917** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 6,878 | 0 | 0 | 0 | **6,878** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 857 | **857** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | 0 | 0 | (5,057) | 0 | 0 | 0 | **(5,057)** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 694 | (694) | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | **0** | **88,431** | **888** | **0** | **2,616** | **101,595** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | **0** | **92,611** | **0** | **0** | **1,597** | **103,868** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 2,571 | 0 | 0 | 0 | **2,571** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | (84) | **(84)** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | 0 | 0 | (10,170) | 0 | 0 | 0 | **(10,170)** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,621) | 1,621 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | **0** | **83,391** | **1,621** | **0** | **1,513** | **96,185** |

## CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

### 1.0 Current Accounts

| Current Accounts | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Required minimum opening balance | Waived | Waived |
| (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 20,000 | USD $20 |
| (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 4,000 | US$ 5.00 |
| (d) Fees per ATM withdrawal | N/A | N/A |
| (e) ATM mini statement | N/A | N/A |
| (f) Interim statement per page | TZS 7,000 | US$ 5.00 |
| (g) Periodic scheduled statement | Waived | Waived |
| (h) Cheque book | TZS 35,000 (100 leaves) | US$ 35 (100 leaves) |
| (i) Dishonoured cheque | TZS 52,000 | US$ 50 |
| (j) Special clearance | TZS 60,000 | US$ 60 |
| (k) Counter cheque | TZS 2,500 per leaf | US$ 2 per leaf |
| (l) Stop Payment | TZS 30,000 | US$ 30 |
| (m) Standing order | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| (n) Balance enquiry | Waived | Waived |
| (o) New ATM card issuance | N/A | N/A |
| (p) ATM card renewal or replacement | N/A | N/A |
| (q) Overdrawn account interest charge | 4.30%-7.55% | 1.38%-7.14% |
| (r) Unarranged overdraft | 15% | 10% |
| (s) Interbank transfer | Waived | Waived |
| (t) Bill payments through ATM | N/A | N/A |
| (u) Deposit fee | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 |
| (v) Other (please specify) | N/A | N/A |
| (w) BRELA Search fees. Per search | TZS 30,000 | US$ 15 |
| (x) Foreign Loan Registration fees (DRN) | US$ 700 | US$ 700 |

### 2.0 Savings Accounts

| Savings Accounts | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Required minimum opening balance | NA | NA |
| (b) Monthly service fee | NA | NA |
| (c) Interim statement | NA | NA |
| (d) Account clossure | NA | NA |

### 3.0 Electronic Banking

| Electronic Banking | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Internet banking monthly fee | Waived | Waived |
| (b) Internet transfers | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.0 and Max US$ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| (c) SMS banking | N/A | N/A |
| (d) Other | Managers Cheques: TZS 4,000 | Managers Cheques: US$ 5.00 |

### 4.0 Foreign Exchange Transactions

| Foreign Exchange Transactions | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | NA | NA |
| (b) Purchase of foreign cheque | NA | NA |
| (c) Sale/purchase of cash passport | NA | NA |
| (d) Telegraphic transfer | | |
| -Inward Telegraphic Transfers [FTIN] | US$ 30 | US$ 30 |
| -Outward International TT / Electronic [ROCT] | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 |
| (e) Telex/SWIFT | NA | NA |
| (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current | NA | NA |

### 5.0 Personal Loans

| Personal Loans | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| (i) Personal loans | NA | NA |
| (ii) Overdrafts | NA | NA |
| (iii) Mortgage finance | NA | NA |
| (iv) Asset finance | NA | NA |
| (b) Unpaid loan instalment | NA | NA |
| (c) Early repayment | NA | NA |
| (d) Valuation fees | NA | NA |
| (e) Other | NA | NA |

### Additional Disclossures

| 1 Deposit Rates | LCY | FCY |
|---|---|---|
| -Current Account Deposits | 0%-3.00% | 0%-0% |
| -Time Deposits | | |
| (a) 1 - Months | 2.73% -2.93% | 0.06%-0.07% |
| (b) 3 - Months | 1.72% -2.02% | 0.12%-0.13% |
| (c) 6 - Months | 2.75% -3.05% | 0.14%-0.16% |
| (d) 9 - Months | 3.04% -3.34% | 0.14%-0.16% |
| (e) 12 - Months | 3.32% -3.62% | 0.21%-0.24% |

| 2 Lending Rate | LCY | FCY |
|---|---|---|
| Base lending rate | 8.55%-9.55% | 3.51%-4.51% |
| Short term ( up to one year ) | 8.55%-9.55% | 3.51%-4.51% |
| Medium term ( 2 to 3 years ) | 9.05%-10.05% | 4.01%-5.01% |
| Long term ( 3 - 5 years ) | 9.55%-10.55% | 4.51%-5.51% |
| Term loans ( over 5 years ) | 10.55%-11.55% | 5.01%-6.01% |

### 6.0 Trade Finance

| Trade Finance | CHARGE/FEE |
|---|---|
| **Documentary Collections** | |
| Imports | Handling: $130, Acceptance $65, Telex: 0.325% minimum $98 and maximum $650 |
| Exports | All in fee: $100 ($50 courier and $50 handling) per set of documents |
| **Imports Letters of Credits** | |
| Opening fees | LC issuance - 0.5% per quarter Min. $325 |
| Handling fees | Handling: $130 |
| Amendment Fees | Simple amendment $100, extension 0.5% per quarter if it extends to other quarter (s) |
| Confirmation fees | Confirmation 0.39% per quarter Min. EUR 390 per quarter |
| Risk margin on Acceptance | 0.25% per Quarter or part thereof |
| Other Bank LC re-issuance | 0.1% per Quarter, min. $200 |
| Bills Availization (Pour Aval) | 0.5% per Quarter or part thereof |
| **Exports Letters of Credits** | |
| Handling fees | $500 |
| Courier | $100 |
| Confirmation fees | 0.25% per Quarter or part thereof |
| Negotiation fees | 0.1% Min. $1000 |
| **Liquidity financing** | |
| Suppliers finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| Accounts Receivable Finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| **Guarantees and Standby Letters of Credits** | |
| SBLC | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Bid Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Performance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Maintanance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Advance Payment Guarantee | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Amendments fees on Guarantees | Simple amendments $100 and 0.5% per Quarter or part thereof, if it extends into next quarter(s) |
| Custom Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Warehouse Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Transit Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Facility fees | 1.5% per annum |

We the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information

| | Name | Designation | | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Iddi Msonga | CFO | ........................................................ | Date : 28th October 2021 |
| 2 | Michael Mungure | TTS Head | ........................................................ | Date : 28th October 2021 |
| 3 | James Rutta | Head of Treasury | ........................................................ | Date : 28th October 2021 |

TANGAZO

# Jiji la Mbeya tunavyomuenzi Mwalimu Nyerere kwa vitendo

**Na Mwandishi Wetu, Mbeya**

Oktoba 14, 1999 Tanzania ilipata pigo baada ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Kwanza na mpigania Uhuru, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kufariki dunia.

Mwalimu alifariki katika Hospitali ya St. Thomas ya nchini Uingereza ambako alikuwa anapatiwa matibabu kutokana na maradhi yaliyokuwa yanamsumbua na taarifa za kifo chake zilizua simanzi na majonzi kwa Watanzania.

Wakati wa uhai wake, Mwalimu Nyerere ambaye alikuwa anaamini siasa za Ujamaa na Kujitegemea, alitangaza maadui watatu ambao walitakiwa kupigwa vita na Watanzania, ambao ni umaskini, ujinga na maradhi.

Katika kukabiliana na maadui hao, Mwalimu aliwahimiza Watanzania kufanya kazi kwa bidii ili kumkabili adui umaskini, kuwapeleka watoto shule ili kumkabili adui ujinga na kuimarisha sekta ya afya ili kumkabili adui maradhi.

Wananchi wa Jiji la Mbeya waliungana kusherehekea na Watanzania wote nchini kote kuadhimisha miaka 22 tangu tuli pompoteza mwanasiasa huyo nguli ambaye fikra na maono yake bado zinaishi.

Katika kuadhimisha siku hiyo, Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa kushirikiana na wananchi tunaendelea kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa kuendeleza mapambano dhidi ya maadui watatu aliohimiza tuwapinge yaani umaskini, ujinga na maradhi.

Tumekuwa tukikabiliana na maadui hawa kwa kushirikiana na Serikali Kuu ambapo kwenye sekta ya afya tumekuwa tukitekeleza mipango ya Serikali ya kuimarisha afya ya msingi.

Kwa sasa jiji letu lina jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 54 vikiwamo vya Serikali, watu binafsi na taasisi za dini na kufanikisha kuwa na zahanati zipo 41, vituo vya afya saba na hospitali sita.

Pamoja na idadi hiyo ya vituo vya kutolea huduma za afya, pia kumekuwa na ongezeko la watu hali ambayo inailazimu Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi pamoja na wadau kuendelea kuboresha miundombinu ya vituo hivyo pamoja na kujenga mipya.

Kwa sasa tunapoadhimisha miaka 22 ya kifo cha Hayati Nyerere, Jiji letu linakadiriwa kuwa na jumla ya watu 500,000 ambao wote wanategemea kupata huduma za afya kwenye vituo hivi tulivyo navyo.

Ili kuongeza ubora wa huduma za afya na kumuenzi vizuri Mwalimu Nyerere, Halmashauri ya Jiji la Mbeya iliamua kujenga Hospitali ya Wilaya kwa kukipandisha hadhi kilichokuwa Kituo cha Afya cha Igawilo.

Ujenzi wa hospitali hiyo mpaka sasa umegharimu Sh. Bilioni 1.65 (1,652,293,760.21) ambazo kati yake Sh. Bilioni 1.5 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu, mapato ya ndani ya Halmashauri ni Sh. Milioni 147.5 (147,507,160.21) na mchango wa wananchi ni Sh. Milioni 4.78 (4,786,600).

Awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali hiyo ulianza Juni 5, 2020 kwa kujenga majengo manne kati ya tisa yaliyokuwa yanahitajika kwenye Hospitali hiyo ambayo ni jengo la wagonjwa wa nnje, Jengo la Maabara, Jengo la kufulia nguo na jengo la Stoo ya dawa.

Muonekano wa Jengo la Wagonjwa wa nje (OPD) la Hospitali ya Igawilo baada ya kupandishwa hadhi kwa hospitai hiyo kutoka kuwa Kituo cha Afya na kuwa Hospitali ya Jiji la Mbeya.



Awamu ya pili ya ujenzi ilianza Aprili 1, 2021 kwa kujenga majengo matano ambayo ni Jengo la Utawala, Jengo la Wodi ya Wazazi, Jengo la Mionzi, Jengo la Mama na Mtoto (RCH) na Wodi ya wanawake.

(Kwenye ujenzi wa majengo yote umefanyika kwa kutumia mfumo wa Account ya dharura (Force account) utaratibu ambao unahimiza matumizi ya mafundi jamii.)

Wakati huu ambao tunaadhimisha miaka 22 ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, ujenzi wa majengo saba ya hospitali hiyo umefikia asilimia 100 na majengo mawili pekee ndiyo yamefikia asilimia (75) kila moja.

Hata hivyo Mradi huo umechelewa kukamilika kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo mvua za masika zilizonyesha mpaka mwezi Juni na kusababisha magari kushindwa kufikisha vifaa vya ujenzi kwenye mradi.

Ili kukabiliana na tatizo hilo baada ya mvua kuisha, tulihimiza mafundi kuongezwa pamoja na vibarua ili mradi ukamilike mapema na wananchi waendelee kupata huduma za afya na tumkabili ipasavyo adui maradhi.

Uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa niaba ya wananchi tunaishukuru Serikali katika awamu zote kwa kutusaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya afya inayotufanya tutembee kwa mafanikio kwenye ndoto za Mwalimu Nyerere.

Tunawatakia Watanzania wote maadhimisho mema ya siku ya kifo cha Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius na tunaahidi kuendelea kumuenzi kwa kutenda yale aliyotuhimiza wakati wa uhai wake.

Muonekano wa Jengo la Mama na Mtoto la Hospitali ya Igawilo ambalo ni miongoni mwa majengo ya Hospitali hiyo yaliyokamilika kwa asilimia 100 na tayari yameanza kutumika.



Mafundi jamii wakiendelea kukamilisha ujenzi wa Jengo la Mionzi la Hospitali ya Jiji la Mbeya ya Igawilo ambalo ni miongoni mwa majengo tisa yaliyojengwa baada ya Hospitali hiyo kupandishwa hadhi kutoka kuwa Kituo cha afya na kuwa Hospitali ya Wilaya.



TANGAZO

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIAKWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka ya sasa Tarehe 30/09/2021 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/06/2021 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 89 | 134 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 11,770 | 11,613 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushungulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima ya Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | | - | - |
| | Mikopo Halisi Iliyopo | 18,166 | 18,137 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,763 | 2,653 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika ,Mitambo na Vifaa | 1,552 | 1,564 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **34,340** | **34,100** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,618 | 1,871 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 3,687 | 3,572 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 798 | 797 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 995 | 922 |
| 27 | Zitakazolipwa Baadae | 1,737 | 1,682 |
| 28 | Dhima Nyingine | - | - |
| **29** | **Madeni** | **8,835** | **8,845** |
| | **JUMLA YA DHIMA** | | |
| **30** | **MALI/(DHIMA)HALISI (16 kutoka 29)** | **25,505** | **25,256** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,200 | 21,200 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 12 | 12 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,259 | 1,259 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 916 | 667 |
| 35 | Akauti Nyingine za Mtaji | 2,118 | 2,118 |
| 36 | **Stahiki ya Wenyehisa Chache** | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISANI** | **25,505** | **25,256** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | **559** | **1,326** |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | **448** | **1,201** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | **-** | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | **74%** | **74%** |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | **3.1%** | **7.3%** |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **342%** | **337%** |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **53%** | **54%** |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **69%** | **71%** |
| (vi) | Ongezeko la Amana | **-2.5%** | **14.1%** |
| (vii) | Ongezeko la Mali | **0.7%** | **3.8%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/09/2021 | Robo ya Mwaka Linganishi 30/09/2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 | Mapato ya Riba | 2,345 | 1,912 | 7,415 | 7,068 |
| 2 | Gharama za Riba | 4 | 12 | 11 | 19 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **2,340** | **1,900** | **7,404** | **7,049** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (70) | **(183)** | (243) | **(857)** |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **542** | **756** | **1,287** | **1,626** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (16) | 1 | (16) | 1 |
| | 6.2 Ada za Kamisheni | 412 | 408 | 877 | 981 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 147 | 347 | 427 | 644 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba :** | **2,511** | **2,450** | **7,374** | **7,985** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 1,193 | 1,195 | 3,615 | 4,081 |
| | 7.2 Gharama Nyingine | 1,318 | 1,255 | 3,759 | 3,905 |
| | 7.3 Ada na Kamisheni | | | | |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **302** | **23** | **1,074** | **(167)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 53 | 55 | 158 | 130 |
| **10** | **Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **249** | **(32)** | **916** | **(298)** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | **263** | **270** | **263** | **270** |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 11,755 | (1,525) | 43,212 | (14,590) |
| 13 | Kipato kwa Hisa | 11,755 | (1,525) | 43,212 | (14,590) |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 | Vituo Vya Biashara | 36 | 54 | 36 | 54 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | 0.7% | -0.1% | 2.7% | -0.8% |
| (ii) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.0% | -0.1% | 3.6% | -1.3% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 87% | 94% | 85% | 94% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalisha | **20%** | **22%** | **62%** | **47%** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2021)** | **21,200** | **1,447** | **0** | **2,206** | **24,853** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **916** | - | - | **916** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | **(188)** | - | **(76)** | **(264)** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **21,200** | **2,176** | **0** | **2,130** | **25,505** |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2020)** | **21,200** | **1,657** | **190** | **2,566** | **25,613** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **(179)** | - | - | **(179)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | **190** | **(190)** | - | - |
| Mengineyo | - | **(220)** | - | **(360)** | **(581)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **1,447** | **0** | **2,205** | **24,853** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/09/2021 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/06/2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/09/2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/09/2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| **I:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| | Mapato/(Hasara)Hakisi | **249** | **220** | **916** | **(298)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | | | |
| | Hasara Katika Mali | 123 | 114 | 345 | 352 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (29) | (1,257) | (2,386) | 5,858 |
| | Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (139) | 673 | 725 | (1,530) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (110) | (38) | 942 | (760) |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo | 129 | 437 | 69 | 1,878 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| | **kwa shughuli za uendeshaji** | **224** | **148** | **611** | **5,500** |
| **II:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | | | | |
| | Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (111) | (51) | (191) | (292) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | | | | |
| | **kwa Shughuli za uekezaji** | **(111)** | (51) | (191) | (292) |
| | | - | - | - | - |
| **III:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | (67) | (264) | (528) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **(67)** | **(264)** | **(528)** |
| **IV:** | **FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | | | | |
| | Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tastimu | 113 | 30 | 156 | 4,680 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 11,746 | 11,716 | 11,703 | 8,622 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu /** | | | | |
| | **Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **11,859** | **11,746** | **11,859** | **13,303** |

Katika kuaandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mwijage B Bishota (Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 15 Oktoba 2021 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha ) | | 15 Oktoba 2021 |
| Modest Kissima (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 15 Oktoba 2021 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1 **Athanasia Soka (Mwenyekiti Wa Bodi)** | | 15 Oktoba 2021 |
| 2 **Loyce Isanzu (Mwendeshaji)** | | 15 Oktoba 2021 |

## ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KUANZIA TAREHE 1 JANUARI 2021

| Huduma za Kibenki | | | Gharama-Pamoja na VAT (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuangalia Salio-Dirishani | | 554 |
| 2 | Kuhamisha fedha | | 944-11,800 |
| 3 | Kutoa disrishani hadi TZS 5,000,000 | | 1,770 |
| 4 | Kubadili Kadi ya ATM | | 11,800 |
| 5 | Taarifa Fupi ATM | | 472 |
| 6 | Gharama za mwezi (Monthly Acc maintanance fees) | Akiba Account | 885 |
| | | Business account | 1,770 |
| 7 | Kufunga Akaunti | Akaunti ya Akiba, Watoto & Dunduliza | 2,360 |
| | | Akaunti ya vikundi na Biashara | 5,900 |
| 8 | Taarifa ya Akaunti | Miezi 0-3 | 1,180 |
| | | Miezi 3-12 | 3,540 |
| | | Miezi 12-24 | 11,800 |
| | | Miezi 24-48 | 29,500 |
| | | Miaka 3-6 | 41,300 |
| | | Zaidi ya miaka 6 | 55,400 |

| Huduma Za Simu (Mobile banking) | | Pamoja na VAT (TZS) |
|---|---|---|
| 9 | Kujua Salio-Simu | 118 |
| 10 | Kutoa-Simu | Bure |
| 11 | Kuhamisha Fedha-Simu | 118 |
| 12 | Taarifa Fupi-Simu | 354 |
| 13 | Kubadili Number ya Siri | 236 |

| Jina na cheo | Signature | Date |
|---|---|---|
| Mwijage B Bishota ( Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu) | Signed | 15-Oct-21 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha ) | Signed | 15-Oct-21 |
| Modest Kissima (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | Signed | 15-Oct-21 |

**Akaunti**

| s/n | Huduma | Kiwango cha chini | Riba Kwa mwaka |
|---|---|---|---|
| 1 | Akiba Accounts | 5,000 | 4% |
| 2 | Joint Accounts | 5,000 | 4% |
| 3 | Group Accounts | 20,000 | 4% |
| 4 | Watoto Accounts | 10,000 | 4% |
| 5 | Bussiness Accounts | 100,000 | 4% |
| 6 | Fixed Deposit Accounts | N/A | Kulingana na muda na Kiasi |
| 7 | Dunduliza Accounts | 10,000 | Kulingana na muda na Kiasi |

**Mikopo ya Vikundi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Biashara Loan | 5% | 60% | 3% |
| 2 | Group Savings Group Loan | 5% | 60% | 2.5% |
| 3 | Group Jiendeleze | 4% | 48% | 3.5% |

**Mikopo Binafsi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Mkopo Binafsi- hadi TZS10M | 4% | 48% | 2.5% |
| 5 | Mkopo Binafsi inayozidi TZS10M Hadi TZS 20M | 3.50% | 42% | 2.5% |
| 6 | Mikopo Binafsi inayozidi TZS20M | 2.50% | 30% | 2.5% |
| 7 | Elimisha | 4% | 48% | 3.5% |

**Mikopo ya Kilimo**

| | Product | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Jikomboe | 4% | 48% | 5% |
| 10 | Jitume | 5% | 60% | 5% |
| 11 | Mkombozi | 5% | 60% | 5% |
| 12 | Patnerships | Negotiable | Negotiable | Negotiable |

## TANGAZO

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED

KCBL Together, Transforming Lives

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30/09/2021
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | A. MALI | Robo mwaka ya sasa 30.09.2021 | Robo mwaka iliyopita 30.06.2021 |
|---|---|---|---|
| 1 | Fedha Taslimu | 133,801 | 120,022 |
| 2 | Salio katika benki kuu ya Tanzania | 548,735 | 484,673 |
| 3 | Uwekezaji katika amana za serikali | - | - |
| 4 | Salio katika benki nyingine na Taasisi za fedha | 3,747,406 | 5,135,561 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizofikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 2,525,510 | 1,602,828 |
| 12 | Mali nyingine | 309,323 | 113,575 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 297,812 | 287,587 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **7,562,587** | **7,744,246** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 4,436,170 | 4,591,360 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalum | - | - |
| 21 | Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | 315 | 3,830 |
| 23 | limbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | 31,642 | 38,629 |
| 24 | Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Fedha za washirika(MIVARF Grant) | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazo lipwa bad | - | - |
| 27 | Dhima nyingine | 357,531 | 653,439 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **4,825,658** | **5,287,258** |
| 30 | **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **2,736,929** | **2,456,988** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 13,950,060 | 13,838,715 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 239,633 | 147,506 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (11,465,253) | (11,553,921) |
| 34 | Faida(hasara)ya kipindi husika | 12,489 | 24,688 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| 37 | **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2,736,929** | **2,456,988** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu | 330,171 | 327,755 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 90,538 | 108,466 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | | |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 36.19% | 31.73% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 12.20% | 17.84% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 60.98% | 40.01% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 33.39% | 20.70% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 33.00% | 20.41% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -3.38% | -10.81% |
| (vii) | Ongezeko la mali | -2.35% | -5.19% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO INAYOISHIA 30/09/2021
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 30/09/2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.09.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.09.2021 | Limbikizo la mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato yariba | 148,144 | 14,715,779 | 390,131 | 42,344 |
| 2 | Gharama za riba | 12,500 | 28,674,907 | 38,913 | 83,765 |
| 3 | Mapato halisi ya riba(1 kutoa 2) | **135,644** | **(13,959,128)** | **351,218** | **(41,421)** |
| 4 | Madeni viza yaliyopitwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | (17,918) | - | (17,918) | - |
| 6 | **Mapato yasiyo ya riba** | **74,091** | **9,863,764** | **217,047** | **112,597** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 33,547 | 5,719,602 | 114,452 | 21,254 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | 40,544 | 4,144,162 | 102,595 | 91,343 |
| 7 | **Gharama zisizo na riba** | **245,018** | **117,116,537** | **568,341** | **502,647** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 123,420 | 72,807,452 | 309,838 | 241,348 |
| | 7.2 Ada na kamishani | 12,179 | - | 12,179 | 20,000 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 109,419 | 44,309,085 | 246,324 | 241,299 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **(17,365)** | **(121,211,901)** | **17,842** | **(431,471)** |
| 9 | **Tengo la kodi ya mapato** | **-** | **0** | **5,353** | **0** |
| 10 | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** - | **(17,365)** | **(121,211,901)** | **12,489** | **(431,471)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisiha)** | | | | |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(17,365)** | **(121,211,901)** | **12,489** | **(431,471)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 24 | 16 | 24 | 16 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | -0.63 | -89.97 | 0.45 | -0.32 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (I ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.23% | -22.34% | 0.50% | -79.52% |
| | (ii) Uwiano wa Faida Baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -1.90% | -6.90% | 1.37% | -23.87% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | 110.25% | -476.48% | 93.60% | -324.41% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | -2.06% | -152.26% | 1.48% | -541.97% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 30/09/2021

| Robo Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Upunguzaji wa jumla wa matengo | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka wa sasa** | 13,838,715 | 0 | -11,529,233 | 147,506 | 0 | 0 | 2,456,988 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 12,489 | | | | 12,489 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 111,345 | | | | | | 111,345 |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | | 92,127 | | | 92,127 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | | | | | 0 |
| Mengineyo | | | 63,980.00 | | | | 63,980 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | **13,950,060** | **-** | **(11,452,764)** | **239,633** | **-** | **-** | **2,736,929** |
| **Robo ya Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka** | **13,761,662** | **-** | **(12,001,566)** | **111,260** | **-** | **-** | **1,871,356** |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 24,688 | | | | 24,688 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | - |
| Miamala na wanahisa | 77,053 | | | | | | 77,053 |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | - |
| Tengo la ziada ya jumla | | | | | | | - |
| Ziada ya kisheria | | | | | | | - |
| Mengineyo | | | 447,645 | 36,246 | | | 483,891 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | **13,838,715** | **-** | **(11,529,233)** | **147,506** | **-** | **-** | **2,456,988** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30/09/2021
(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka kwa sasa 30.09.2021 | Robo mwaka iliyopita 30.06.2021 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (17,365) | 8,451 |
| | **Marekebisho Kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Badiliko katika mali isiyoshikika | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 10,225 | (3,545) |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | (922,682) | (610,250) |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika amana | (155,190) | (556,666) |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (295,907) | 71,217 |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | (195,748) | (7,874) |
| | - Kodi iliyolipwa | (12,340) | (62,053) |
| | - Mengineyo(bainisha) | 167,348 | 57,315 |
| | - Maslahi ya wachache | | 1,611 |
| | - Madeni na benki nyingine | - | - |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji*** | **(1,421,659)** | **(1,101,794)** |
| II: | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | - | - |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji*** | - | - |
| III: | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | 111,345 | 56,403 |
| | Gawio lililolipwa kwa fedha taslimu | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | - | - |
| | Mengnineyo | - | - |
| | ***Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha*** | **111,345** | **56,403** |
| IV: | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu:** | | |
| | **Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali** | **(1,310,314)** | **(1,045,391)** |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo ya mwaka.** | **5,740,256** | **6,785,647** |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo ya mwaka.** | **4,429,942** | **5,740,256** |

| *JINA NA CHEO* | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| Godfrey J. Ng'urah<br>**MANEJA MKUU** | Imesainiwa | 29/10/ 2021 |
| Apolinary S. Kityamwi<br>**MKUU WA UKAGUZI WA NDANI** | Imesainiwa | 29/10/2021 |
| Anthony B. Bichakila<br>**MKUU WA FEDHA NA UTAWALA** | Imesainiwa | 29/10/2021 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini ,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu ,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

| *JINA NA CHEO* | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| 1. **Dr GERVAS M. MACHIMU, MWENYEKITI WA BODI** | Imesainiwa | 29/10/2021 |
| 2. **MRS. CHIKU ISSA ,MWENYEKITI WA BODI MSAIDIZI** | Imesainiwa | 29/10/2021 |

### MINIMUM DISLOSURES OF CHARGES AND FEES

| NUMBER | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1.0 | **Current Accounts** | |
| | Monthly service fee: | |
| | Individuals | 13,000 |
| | Umoja Account | 10,000 |
| | Jasiri Account | 7,500 |
| | Fees per ATM withdrawal | 1,500 |
| | ATM balance inquiry | 500 |
| | Interim statement per page | 1,000 |
| | Cheque book 100 leaf. | 50,000 |
| | Dishonoured cheque | 1% min.150,000 max.300,000 |
| | Stop payment | 1% min.50,000 max.300,000 |
| | Bulk payment processing fee - charged to beneficiary | 1,000 |
| | Standing order | free |
| | Balance enquiry over the counter | 300 |
| | ATM card annual maintanance fee | 13,558 |
| | ATM card replacement renewal | 9,999 |
| | ATM card replacement lost/spoilt | 9,999 |
| | Withdraw fees | |
| | Umoja Account | 2,000 |
| | Below 3,000,000 | 3,000 |
| | 3,000,000-4,999,999 | 5,000 |
| | 5,000,000-24,999,999 | 10,000 |
| | Above 25,000,000 | 0.25% |
| 2.0 | **Savings Accounts** | |
| | Monthly service fee | 1,800 |
| | ATM withdrawal fee | 1,500 |

| | | |
|---|---|---|
| | Cash withdraw fees | |
| | 1,000-499,999 | 2,000 |
| | 500,000-999,999 | 3,000 |
| | 1,000,000-2,999,999 | 4,000 |
| | 3,000,000-4,999,999 | 5,000 |
| | 5,000,000-Above | 0.25% |
| | Salary processing fee | 3,000 |
| 3.0 | **Electronic Banking** | |
| | Other TT/SWIFT | 10,000 |
| 4.0 | **Loan fees** | |
| | Application fees | |
| | Amcos and Saccos | 1.5% |
| | MSME-up to 100 mn | 0.5% min 100,000 |
| | SME-101MN-1BN | 0.5% min 1,000,000 Max 5,000,000 |
| | Facility fees | |
| | Amcos and Saccos | 1.0% |
| | Individuals | 1.0% |
| | Personal loans | 1.8% |
| 5.0 | **Lending rates** | |
| | Amcos and Saccos | 17% |
| | MSME | 18% |
| | Personal Loans | 15% |
| | Mama Africa | 14% |
| 6.0 | **Interest on deposit** | |
| | Minimum balance for saving | 50,000 |
| | Minimum balance for FDR | 200,000 |
| | Interest on deposit | 1% |
| | Interest on FDR | 3-5% |
| | We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information. NB:All charges are VAT exclusive. | |

| | *JINA NA CHEO* | | SAHIHI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Godfrey J. Ng'urah | MENEJA MKUU | | 29/10/2021 |
| 2 | Apolinary S. Kityamwi | MKUU WA UKAGUZI WA NDANI | Imesainiwa | 29/10/2021 |
| 3 | Anthony B. Bichakila | MKUU WA FEDHA NA UTAWALA | Imesainiwa | 29/10/2021 |

| | *Name and Title* | SAHIHI | TAREHE |
|---|---|---|---|
| 1 | **Dr GERVAS M. MACHIMU, MWENYEKITI WA BODI** | Imesainiwa | 29/10/2021 |
| 2 | **MRS. CHIKU ISSA,MWENYEKITI WA BODI MSAIDIZI** | Imesainiwa | 29/10/2021 |





## Wizara yaanza utafiti wa corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeanza kufanya utafiti sita wa kitaalamu kuhusu virusi vya corona ikiwamo kupima watu waliopata chanjo ili kubaini kiwango cha kinga walichopata.

Uafiti mwingine ni uelewa, mtazamo na utendaji, utafiti wa kimatibabu, kuchunguza mpangilio wa vinasaba, hali ya kimelea kubadili hali, vinasaba vyake vya awali na utafiti wa tiba asili ambapo kiasi cha Sh. bilioni 15.9 zitatumika.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa kuhusu matumizi ya Sh. bilioni 259.2 kati ya Sh. trilioni 1.3 zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya utekelezaji wa mapambano dhidi ya UVIKO-19, kwa wizara hiyo.

Alisema matokeo ya tafiti hizo, yatawezesha serikali kufahamu aina ya kirusi kilichoko nchini ili kufanya vipimo na kutoa chanjo.

"Kufahamu sababu za mwitikio mdogo wa jamii katika kupata chanjo ya UVIKO - 19 hivyo kuishauri serikali njia sahihi ya kuongeza mwitikio kufahamu ufanisi wa dawa za asili katika kupambana na UVIKO - 19 na kuishauri serikali," alisema.

Pia, alisema tafiti hizo zitasaidia kufahamu madhara ya UVIKO - 19 kwa wagonjwa wanaopata maambukizi, kufahamu viambata vilivyopo kwenye dawa za asili ambavyo hutibu corona na kufanya ugunduzi wa chanjo dhidi ya UVIKO-19.

"Utafiti huu wa kuwa na chanjo yetu tutaufanya kwa kushirikiana na magwiji kutoka Hospitali ya Muhimbili pamoja na Chuo cha Sua kwani kama hawa wataalamu wetu tayari walishagundua chanjo ya mifugo kwanini tusiwekeze nguvu kupata chanjo ya yetu ya UVIKO-19," alisema Prof. Makubi.

Aliongeza kuwa kupitia fedha hizo kutaimarisha huduma za dharura, wagonjwa mahututi na wanaohitaji uangalizi maalum itakayogharimu Sh. bilioni 254.4.

"Uwekezaji huu unategemewa kupunguza vifo vya wagonjwa kwa asilimia 20 - 40% ndani ya vituo vya afya, kuimarisha huduma za maabara, mionzi na tiba mtandao itakayogharimu Sh. bilioni 111.5," alisema.

Aidha, alisema hali hiyo itasaidia ugunduzi wa haraka wa magonjwa mbalimbali na kupunguza rufani kwenda Hospitali ya Taifa.

Vilevile, alisema hali hiyo itaimarisha huduma za chanjo dhidi ya UVIKO - 19 na elimu ya afya kwa umma dhidi ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 43.2.

"Hivyo tutaweza kuwakinga wananchi wengi dhidi ya vifo vinavyohusiana na UVIKO-19," alisema.

Kadhalika, alisema kuwa fedha hizo zitasaidia kuimarisha miundombinu katika vituo vya kutolea huduma za afya itakayogharimu Sh. bilioni 41.8 na kupanua na kuboresha huduma za kibingwa katika ngazi ya mikoa na kanda.

# Serikali yaombwa sheria dhidi ukatili wa kijinsia

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kutunga sheria mahsusi ya kusimamia masuala ya ukatili wa kijinsia nchini ili kuondoa mkanganyiko wa tafsiri za baadhi ya sheria zilizopo.

Mratibu wa Mradi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Wakili Josephine Anold, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja kwa maofisa wa serikali kutoka wizara mbalimbali.

Alisema: "Hatusemi kuwa hakuna kabisa sheria za kutetea mambo ya kijinsia lakini bado kuna mkanganyiko katika tafsiri za baadhi ya sheria za makundi ya kijinsia yaliyopo nchini."

Alibanisha kuwa kuanzishwa kwa sheria hiyo itasaidia kutafsiri vizuri aina ya ukatili pamoja na kuainisha adhabu kwa mhusika aliyetenda kosa na mtendewa.

Kadhalika, alisema kuna makundi mengi ya kijinsia ambayo ni pamoja na watoto ambao kwa sasa kuna sheria iliyotungwa na kutoa tafsiri ya mtoto ni nani na umri sahihi wa kumtambua mtoto. Wakili Anold alisema sheria ya makosa ya kujamiiana ilisaidia kupunguza makosa ya vitendo vya ubakaji vilivyokuwa wakifanyiwa baadhi ya wanawake.

Alisema bado kuna vitendo vya ukatili vinafanyika kwenye jamii kwa kunyanyasana hasa kwa wanandoa hivyo ukatili huo umekuwa ukiwaathiri miongoni mwao na kusababisha kuathiri familia.

"Ukatili unaweza kufanywa na mtu yeyote inaweza kutokea mwanaume kumnyanyasa mwanamke au mwanamke kumnyanyasa mwanaume wote hawa wanahitaji sheria ya kuwalinda ili kila mtu apate haki yake," alisema.

Aidha, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo maofisa hao wa serikali ili kupaza sauti katika maeneo yao ya kazi kwa lengo la kukomesha vitendo vya ukatili mahali pa kazi na nyumbani.

Aliongeza kuwa chama hicho kinatekeleza mradi wenye lengo la kuongeza ushiriki na uwakilishi wa wanawake na vijana katika shughuli za kisiasa na uongozi katika ngazi mbalimbali.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa TAWLA, Tike Mwambipile, alisema kwa sasa inafanyakazi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Mwanza, Arusha na Mbeya, lakini kwa mikoa mingine wanafanyakazi kwa kutumia wasaidizi wa sheria.



Mratibu wa Mradi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Wakili Josephine Anold (kulia), akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya siku moja kwa maofisa kutoka wizara mbalimbali, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Maandalizi rasmi mpango kazi amani, usalama wa wanawake

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, amefungua kikao kazi cha kuandaa mpango kazi wa taifa wa masuala ya amani, usalama wa wanawake na usalama wa wanawake nchini.

Kikao hicho kinachotekeleza azimio la Umoja wa Mataifa la kila nchi mwanachama kuandaa mpango kazi kwa lengo la ushiriki wa wanawake kwenye michakato ya ulinzi na usalama na kuwalinda wanawake kwenye migogoro.

Akizungumza katika kikao hicho kinafanyika kwa siku mbili jijini Dodoma, Dk. Jingu, alisema katika utatuzi wa migogoro, wanawake wana nafasi kubwa hivyo, azimio hilo lilikuwa ni mapinduzi makubwa kwa kutambua kuwa kwenye migogoro kuna masuala ya kijinsia.

"Wanawake wamekuwa ni waathirika wakubwa hususani kwenye vita, unyanyasaji wa kingono hutumika kama silaha kuwaadhibu jamii nyingine, ambapo vitendo vya ubakaji huathiri wanawake kwa kiwango kikubwa kuliko wanaume," alisema.

Aliongeza: "Sisi katika nchi yetu kwenye mambo yote wamekuwa wakishiriki na yamezingatiwa, lakini ili kutekeleza vizuri haya mambo lazima iundwe kikosi kazi ili kwenda pamoja."

Dk. Jingu kuwa, kama nchi na sehemu ya jamii ya Umoja wa Kitaifa lazima kutekeleza azimio hilo kwa kuzingatia historia, uzoefu, taratibu na mila na desturi.

Aidha, aliishukuru Taasisi ya Mwalimu Nyerere kwa kuungana kushiriki kutengeneza mpango kazi huo kwani itaongeza mawazo ya uzoefu kufanikisha jambo hilo na kuwahakikishia kikosi hicho kuwa, serikali kupitia wizara itashiriki kikamilifu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, alisema jamii inatakiwa kuwaheshimu wanawake na tangu wakati wa Muungano wametakiwa wakitambua watu wote wana haki sawa, hivyo usawa ni jambo la kuzingatia.

"Mpango kazi huu utakoandaliwa utazingatia mipango na mikakati inayoleta usawa baina ya jinsi zote ni muhimu kwa mstakabali wa maendeleo ya jamii," alisema Butiku.

Naye mshauri mbobezi wa masuala ya sera na mipango wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN Women), Usu Malya, alisema masuala yaliyopo kwenye azimio la Umoja wa Mataifa ambayo yanalenga ushiriki wa wanawake kwenye kuzuia migogoro yatazingatiwa na Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kushirikisha wanawake kwenye nyanja nyingi ikiwamo uongozi, elimu, uchumi na migogoro hivyo mpango kazi utaweza kuongoza vema masuala hayo kwa utaratibu mzuri.





# Waomba kuboreshewa mashine kuvunia mpunga

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga katika skimu ya umwagiliaji ya Mbuyuni Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wameiomba serikali na wadau wa kilimo kuwasaidia kuboresha mashine za kuvunia mpunga.

Lengo ni kuepusha upotevu wa mazao unaotokana na kuchelewa kuvuna mpunga.

Walitoa ombi hilo wakati wa ziara ya kukagua miradi ya kilimo na mifugo iliyofanywa na maofisa wa Taasisi isiyokuwa ya kiserikali inayohusika na mambo ya kilimo ya Agricultural Non-State Actors Forum (ANSAF) na maofisa wa Mtandao wa Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali Mkoa wa Mbeya (Mbengonet).

Mwenyekiti wa Skimu hiyo, Fashon Madege, alisema mwaka 2015 serikali iliwapatia mashine 11 za kuvunia mpunga, lakini mpaka sasa wamebaki na mashine tatu pekee zinazofanya kazi, hali ambayo imepunguza ufanisi wa uvunaji.

Alisema kati ya mashine hizo 11 Halmashauri ya Mbarali ilizichukua tatu na hawajui zilipelekwa wapi, mbili zilishindwa kufanya kazi kutokana na teknolojia ya matengenezo yake kushindwa kuendana na mazingira kutoendana na mazingira na tatu zimeharibika.

Alisema kati ya mashine hizo tatu zilizoharibika ni moja pekee ndiyo inayotengenezeka, lakini bado wameshindwa kuitengeneza kutokana na kutokuwa na uwezo wa kiuchumi.

"Tunaomba kama inawezekana serikali itusaidie kununua mashine za kuvunia za kisasa, kwa sasa zimekuja mashine ambazo ni za kisasa na zinasababisha za kwetu kukosa soko, kwa sasa tunaomba serikali itusaidie kuboresha mashine hizi," alisema Mdege.

Vilevile aliomba serikali iwasaidie kuboresha mashine yao ya kukoboa mpunga, akisema uendeshaji wake ni mgumu kutokana na kutumia umeme mwingi tofauti na mashine zingine.

Katibu wa Kamati ya ufuatiliaji wa miradi wa Mbengonet Wilaya ya Mbarali, Elisha Mwanikawaga, alisema ufuatiliaji wa miradi wa kamati hiyo ulibaini kuwa kutelekezwa kwa mashine hizo kunaisababishia serikali hasara kubwa.

Alisema kwa mazingira ya Wilaya ya Mbarali yalivyo yanatakiwa mashine aina ya Cubota ambazo ndizo zinavumilia shuruba lakini zingine hazina uwezo wa kuhimili.

Alisema pamoja na mashine hizo, pia Serikali inatakiwa kuwasaidia wananchi hao kuboresha Skimu yao ya umwagiliaji kwa kusakafia mfereji ili kuepusha upotevu wa maji kabla hayajafika mashambani.

"Kitu kingine tulichokibaini ni kwamba wananchi hawa walikabidhiwa mashine hizi bila mandishi yoyote na hata zile mbili zilizochukuliwa hazikuchukuliwa kwa mandishi, hivyo tunaomba utaratibu huu uboreshwe," alisema Mwanikawaga.

Mratibu wa Usangonet, Terdy Mhagama, alisema skimu nyingi za wilaya hiyo zinakabiliwa na matatizo mengi ambayo walibaini kuwa yanakwamisha maendeleo ya skimu na vyama vya ushirika.

Alisema katika skimu hiyo pia kuna tatizo la migogoro kati ya wakulima na wafugaji kutokana na baadhi ya wafugaji kuingiza mifugo kwenye maeneo ya skimu na kusababisha mifereji kufukiwa na hata mazao kuliwa na mifugo.



Ng'ombe wakivuka kwenye mfereji wa maji wa skimu ya umwagiliaji ya Isenyela wilayani Mbarali, mkoani Mbeya juzi, kitendo ambacho kinadaiwa kusababisha migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima wa eneo hilo na wafugaji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# NACOPHA yapiga jeki mapambano ya corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARAZA la Taifa la Watu wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), kupitia mradi wake wa 'Hebu Tuyajenge' chini ya ufadhili wa Shirika la misaada la watu wa Marekani, limetoa vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona kwa wanachama wake wa Mkoa wa Mbeya.

Aidha, baraza hilo limewahamasisha wanachama wake kupata chanjo ya kujikinga na corona ambayo inatolewa bure na serikali, huku likiwataka kuchukua tahadhari mbalimbali zinazoshauriwa na wataalamu wa afya kujikinga na ugonjwa huo.

Vifaa vya kujikinga na corona vilivyotolewa na baraza hilo kwa wanachama ni ndoo za maji tiririka, sabuni za kunawia mikono, vitakasa mikono na barakoa.

Akikabidhi vifaa hivyo juzi katika Ofisi za Konga ya Jiji la Mbeya, Meneja wa NACOPHA Kanda ya Mbeya, Ferdinand Mazuni, alisema vifaa hivyo vimetolewa na baraza hilo katika halmashauri zote nchini ambazo zinatekeleza Mradi wa Hebu Tuyajenge.

Alisema kwa Mkoa wa Mbeya mradi huo unatekelezwa katika halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Rungwe na kwamba vifaa hivyo ni muhimu katika kukabiliana na janga hilo la corona.

"Sisi kama baraza vita dhidi ya corona tulianza nayo tangu ugonjwa huu ulipoanza, tulianza kutoa elimu kwa watu wetu na hata kutoa vifaa vya kujikinga, lakini kwa sasa baada ya mfadhili wetu kutusaidia tumeona ni vema tugawe vifaa hivi kwa wenzetu," alisema Mazuni.

Mwenyekiti wa Konga ya Jiji la Mbeya, Deogratius Kisunga, alisema vifaa vilivyotolewa vitawanufaisha zaidi ya watu 3,000 wa Jiji hilo wanaoishi na Virusi vya Ukimwi, na kwamba vitagawiwa kwenye vikundi vilivyopo katika kila kata.

Aliushukuru uongozi wa Baraza hilo Taifa kwa kutoa vifaa hivyo akisema kuwa vitawasaidia kujikinga na virusi hivyo, huku akiwataka wanufaika kuhakikisha wanavitumia ipasavyo.

Aliwataka wanachama wote kuepuka upotoshaji unaoenezwa na baadhi ya watu kuhusu chanjo ya corona kwa maelezo kuwa watu hao wana nia ovu ya kurudisha nyuma juhudi za serikali kwenye vita dhidi ya ugonjwa huo.

"Kinachosikitisha ni kwamba wanaosema vibaya kuhusu chanjo ni wale ambao hawajachanja, waliochanja wanasema chanjo haina madhara sasa ninachowashauri ni kwamba tuwasikilize wataalamu wa afya badala ya kuwasikiliza wapotoshaji hawa," alisema Kisunga.

Aliwataka watu wote wanaoishi na Virusi vya Ukimwi kuhakikisha wanachanjwa chanjo ya corona ili kuimarisha kinga za miili yao na kwamba chanjo hiyo mpaka sasa inatolewa kwa hiari.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake wanaoishi na VVU Tanzania, Joceline Mtono, aliwataka wanawake kuchangamkia fursa ya chanjo ili wawe salama.

# Songwe wapewa elimu kilimo bora

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAKAZI sita wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, wamepatiwa elimu ya kilimo bora, kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa chakula kuepuka kukumbwa na njaa.

Aidha, wananchi hao wamepatiwa elimu ya uhifadhi wa chakula ili kuepuka upotevu wa mazao yao baada ya kuvuna unaotokana na kuoza ama kuliwa na wadudu.

Elimu hiyo ilitolewa mwishoni mwa juzi na Shirika la Maendeleo la ADP Mbozi, ambalo liliamua kuanzisha programu hiyo ya kutoa elimu kwa wakulima wa eneo hilo ili kuwanusuru na tatizo la njaa ambalo linadaiwa kuwa sugu.

Mkurugenzi wa Shirika la ADP Mbozi, Daria Rugumira, alisema wakulima wa eneo hilo wamekuwa wakizalisha chakula kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na mahitaji yao hali ambayo ndiyo ilikuwa inakuwa chanzo cha njaa.

Aidha, alisema wananchi hao wamekuwa wakiuza sehemu kubwa ya mazao yao ili kupata fedha za kujikimu na hivyo kubaki na kiasi kidogo cha chakula.

"Tunataka kuwasaidia wakulima hawa ili waongeze uzalishaji na wawe na uwezo mkubwa wa kutunza chakula kwa ajili ya matumizi, tumeshalibaini tatizo lao na ndiomaana tumeamua kuwasaidia elimu ya kukabiliana na tatizo hili," alisema Rugumira.

Baadhi ya wananchi waliopatiwa elimu hiyo kuanzia uzalishaji shambani hadi kuhifadhi chakula majumbani walisema elimu hiyo itawanufaisha kwa kiasi kikubwa wakidai kuwa walifundishwa vitu vingi vinavyohusiana na kilimo.

Mmoja wa wananchi hao, Anna Nzuwa, alisema kwa muda mrefu walikuwa wanakumbwa na njaa kutokana na uzalishaji kuwa mdogo na kuhifadhi chakula kwa kutumia njia ambazo zilikuwa zinasababisha chakula kuharibika.

Alisema baada ya kupata elimu hiyo sasa wataondokana na tatizo la njaa na watakuwa na uhakika wa kuhifadhi chakula cha kutumia mwaka mzima.

"Hizi mbinu za kutunza chakula ni nzuri sana kwetu na nina uhakika zitakuwa suluhisho, tulikuwa tunabaki bila akiba kwa sababu uzalishaji ulikuwa chini na tulikuwa tunauza sana," alisema Anna.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Galula, John Ntakoma, alisema serikali ya wilaya hiyo itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuboresha uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Alilishukuru shirika hilo kwa kazi ambayo linafanya ya kuelimisha wananchi, akisema elimu wanayopata itawasaidia wananchi kuongeza uzalishaji.





# Makamu Rais ashtukia uharibifu wa mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni vyema miradi mkubwa ya maendeleo, hasa ya ujenzi wa miradi ya uwekezaji inayoanzishwa, kufanyiwa tathmini ya kina ili kujua uhitaji halisi wa mchanga na kuwekewa mipango na utaratibu bora utakaosaidia kupunguza athari za uchafuzi wa mazingira Zanzibar.

Othman aliyasema hayo jana katika Jumba la Wananchi Forodhani mjini Unguja, alipozungumza na watendaji wa mikoa, wilaya na Idara ya Mazingira katika mkutano wa majumuisho na tathmini ya ziara yake ya kimazingira aliyoifanya hivi karibuni katika mikoa mitatu ya Unguja.

Alisema katika ziara hiyo, amebaini hali ya mazingira katika maeneo mengi aliyotembelea ni mbaya kutokana na uchimbaji holela wa mchanga na mawe unaofanywa na vijana.

Alisema kufanyika kwa tathmini ya uhitaji wa matumizi ya rasilimali hiyo kwa miradi ya aina hiyo kabla ya kuanzishwa ni muhimu na kutaiwezesha serikali kuwa na mpango rasmi na madhubuti utakaosaidia kuandaa sera ya kudhibiti hali hiyo na kunusuru mazingira yasiendelee kuharibika.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia serikali kuwa na mwelekeo mpya katika kusimamia suala la kupambana na uharibifu wa mazingira unaotokana na mabadiliko ya tabia nchi na shughuli zinazofanywa na binaadamu.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwashauri wawekezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayohusisha matumizi ya mchanga, kuagiza rasilimali hiyo kutoka nje ya Zanzibar.

Kiongozi huyo alisema kuwa katika ziara hiyo pia amebaini Mkoa wa Kusini Unguja ndio ulioathirika zaidi na uchimbaji wa mchanga holela hasa katika eneo la Bungi na kuwataka watendaji wa wilaya na ngazi ya mkoa kutafakari zaidi mbinu sahihi ya kudhibiti hali hiyo isiendelee kutokea.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa, alishauri kuwapo jitihada kubwa za kuyafukia maeneo yote yaliyoaharibika ili kuyarejesha katika hali yake ya asili.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohmad Mahmoud, alisema kuna haja kudhibiti wachimbaji wadogo wa mchanga kwa kuwawekea utaratibu maalum kwa kuwa wamekuwa wakichangia kasi kubwa ya uharibifu wa mazingira nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid, alikiri eneo la Bungi kuharibiwa vibaya na uchimbaji wa mchanga holela na kwamba wananchi wa eneo hilo wamekuwa wakiwaficha wahalifu wanaoharibu mazingira katika eneo hilo.

Alishauri kuwapo kambi maalum ya ulinzi katika eneo la Bungi ili kuwadhibiti vijana wanaoendelea kufanya uharibifu huo.

## Kamati za maafa za shehia kunolewa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa kushirikiana na maofisa wa Kikosi cha Zimamoto Zanzibar, inakusudia kuanza kutoa mafunzo ya kujikinga na majanga ya moto kwa kamati za maafa za shehia zilizomo ndani ya wilaya hiyo kwa lengo la kudhibiti majanga pindi yatakapotokea.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Haji Khatib Haji, alibainisha hayo jana katika Shule ya Kusini Makunduchi wakati wa utoaji wa mafunzo ya vitendo kwa wajumbe wa kamati za maafa wa shehia za Mzuri na Tasani, Wilaya ya Kusini.

Alisema halmashauri hiyo imeona upo umuhimu mkubwa wa kutoa mafunzo hayo kwa jamii baada ya kuona hawana uelewa wa kutosha wa kujikinga na majanga mbalimbali yakiwamo ya moto.

Ofisa huyo alisema kutolewa kwa mafunzo hayo kutasaidia kwa kiasi kikubwa jamii kujikinga na maafa yatokanayo na majanga hayo.

Vilevile, alisema mafunzo kama hayo pia wanatarajia kuyatoa katika shehia 21 za wilaya hiyo pamoja na maeneo ya wawekezaji, zikiwamo hoteli za kitalii, maeneo ya wavuvi, masoko na kwa wakulima ambapo maeneo hayo yameonekana kuathiriwa zaidi na majanga ya moto.

Sajent Muhidini Mzee kutoka Kikosi cha Zimamoto Kitengo cha Mafunzo, alisema hatua iliyochukuliwa na halmashauri hiyo inafaa kuigwa na taasisi zengine huku akisisitiza jamii kujenga tabia ya kutoa taarifa mapema katika vyombo husika pale majanga yanapotokea kwa lengo la kunusuru maisha ya watu na mali zao.

Washiriki wa mafunzo hayo walishauri kusambazwa kwa vifaa vya kuzimia moto katika maeneo hatarishi ili kurahisisha kazi ya udhibiti wa majanga ya moto pindi tu yanapotokea.



Mtoto Said Juma akichambua karafuu nje ya kituo cha uuzaji wa zao hilo, mkoani Pemba jana. Watoto wengi wenye umri wa kuwa shule wamekuwa wakijihusisha na vibarua vya kuchambua karafuu hasa wakati wa msimu wa zao hilo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Chuo chatoa mwanga maendeleo Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwapo kwa shughuli za Africa College of Insuarance and Social Protection, kutasaidia Zanzibar kuwa kitovu cha biashara na masuala mbalimbali ya kiuchumi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi alipozungumza na uongozi wa chuo hicho Ikulu Zanzibar, akisema serikali itashirikiana na kufanya kazi pamoja na chuo hicho na ipo tayari kuanzishwa kituo cha kuwajengea uwezo wataalamu.

Rais Mwinyi pia aliridhia ombi la kuwa mgeni rasmi katika mkutano wa mashirika ya bima Afrika unaotarajiwa kufanyika Zanzibar kati ya Januari 26 na 28 mwakani, ambapo washiriki zaidi ya 300 kutoka mataifa mbalimbali duniani watahudhuria.

Alisema kufanyika kwa mkutano huo kutatoa fursa kwa washiriki kuona vivutio mbalimbali vilivyopo Zanzibar na hivyo kuutangaza utalii wa Zanzibar.

Mwenyekiti Mtendaji wa Chuo hicho, Dk. Baghayo Abdalla Saqware, aliiomba serikali kushirikiana na chuo ili kuanzisha kituo kitakachofundisha wataalamu katika masuala ya fedha.

Alisema hatua hiyo itatoa fursa kwa mashirika mbalimbali duniani kuanzisha ofisi zake nchini.

Akizungumzia kufanyika kwa mkutano wa mashirika ya bima Afrika, Saqware alisema pamoja na mambo mengine, washiriki wa mkutano huo watapata fursa ya kujadili shughuli za kibiashara zilivyofanyika mwaka 2021.

Chuo cha Afrika College of Insuarance & Social Protection kilichopo jijini Dar es Salaam, kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha elimu, kazi na teknolojia pamoja na kuyatafutia ufumbuzi masuala mbalimbali katika sekta za fedha na masuala ya kijamii.

# Shule binafsi zapewa mbinu utunzaji fedha

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE binafsi nchini zimetakiwa kuwafundisha elimu ya kutunza fedha wanafunzi tangu wakiwa wadogo ili waje kuwa wajasiriamali wakubwa na mahiri wanapomaliza masomo yao ya elimu ya juu.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, wakati akifungua mkutano mkuu wa tatu wa Chama cha Wawekezaji Binafsi katika Elimu (TAPIE).

"Huwezi kuwa mjasiriamali mzuri kama hujui kutunza fedha, sasa wafundisheni umuhimu wa kutunza fedha na wafungulieni akaunti hii itawajengea utamaduni mzuri wakiwa wakubwa," alisema Abdulumajid.

Pia alipongeza shule binafsi kwa kuendelea kufanya vizuri kitaaluma na aliipongeza pia serikali akisema kuwa kufanya vizuri kwa sekta binafsi katika elimu ni matokeo ya jitihada za serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa sekta hiyo.

Alisema kufanya vizuri kwa shule nyingi binafsi kumewavutia wazazi wengi kuwapeleka watoto wao kwenye shule hizo hata pale wanapofaulu kujiunga na shule mbalimbali za umma.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa elimu, Benki ya CRDB imeiweka sekta ya elimu kama kipaumbele kwa kuendelea kuiwezesha kwa mikopo na mitaji.

Nsekela alisema mwaka jana na nusu ya mwaka huu shule nyingi zilipata shida kutokana na janga la Covid-19, lakini benki hiyo iliweka mazingira rafiki kwa kuhakikisha wenye shule wanapewa muda mwingi wa kulipa mikopo.

"Shule nyingi zilikuwa kwenye mapumziko kutokana na janga hilo hivyo hali ya uchumi haikuwa nzuri kwao, lakini sisi tuliwapitia mmoja baada ya mwingine kuangalia changamoto yake na kutafuta suluhu," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TAPIE, Mahmoud Mringo, aliomba benki mbalimbali zipunguze riba ya mikopo ili kuwawezesha wamiliki wa shule kupata mikopo nafuu.

Alisema uwekezaji kwenye elimu unachukua muda mrefu kurejesha faida, lakini wamekuwa wakipata vikwazo kupata mikopo ikiwamo viwango vikubwa vya riba.

Alisema shule binafsi zimekuwa zikitozwa tozo mbalimbali za serikali na kuwa na mzigo mkubwa wa kujiendesha hali inayowafanya wenye shule wengi kuishi wakiwa na msongo wa mawazo.

# UDOM yamsimamisha mtumishi kwa tuhuma za rushwa ya ngono

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UONGOZI wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), umemsimamisha kazi mtumishi wake (Jina limehifadhiwa) kwa tuhuma za kujihusisha na rushwa ya ngono kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na uongozi wa chuo hicho jana, Oktoba 25, 2021 kilipokea kwa masikitiko taarifa za tuhuma, dhidi ya mtumishi wake huyo kujihusishja na rushwa ya ngono kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

"Baada ya kupokea taarifa hizo chuo kimeanzisha mchakato wa hatua za kinidhamu na maadili kulingana na sheria na kanuni za utumishi wa umma," ilibainisha sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilisema mtumishi huyo alisimamishwa kufanya majukumu yake yote yakiwamo kufundisha kuanzia Oktoba 25, mwaka huu hadi hapo uchunguzi utakapo kamilika.

"Chuo Kikuu cha Dodoma kimekuwa kikichukua hatua stahiki za kinidhamu kwa mujibu wa sheria na taratibu za utumishi wa umma bila kumuonea mtumishi yeyote," ilisema taarifa hiyo.

Vilevile, taarifa hiyo ilisema chuo kina utaarifu umma kuwa kitendo hicho hakivumiliki wala kukubalika na kwamba wakati wote kitaendelea kusimamia nidhamu na maadili kwa watumishi wake wote.

"Pia chuo kitaendelea kuchukua hatua kali kwa mtumishi yeyote atakayebainika kujihusisha na makosa ya kinidhamu," ilifafanua taarifa hiyo.



Mwanzilishi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa mradi wa ubunifu wa Ndoto Hub, Faraja Nyalandu, akichangia mada kwenye mkutano wa wadau wa ubunifu ulioandaliwa na mradi wa ubunifu wa Funguo Hub, mkoani Arusha juzi na kushirikisha wadau mbalimbali wa ubunifu nchini, Funguo Hub inadhaminiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Watu wanne wafariki dunia ajalini

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WATU wanne wamefariki dunia na wengine kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi lililokuwa likitokea Mwanza kugongana na lori.

Kwa mujibu wa taarifa iliyothibitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Iringa, basi hilo la Kampuni ya Isamilo lenye namba za usajili T 398 BNH liligongana na gari lori lenye namba T760 BBY, juzi wakati likitokea Mwanza kuelekea Iringa.

Alisema lori hilo la kampuni ya Justas Investment Co Limited lililokuwa likitokea Iringa, dereva wake alikimbia baada ya ajali hiyo.

Aliwataja waliofariki katika ajali hiyo kuwa mi Gerald John, Happy Kwangu, Edger aliyetambulika kwa jina moja na abiria mmoja ambaye bado hajafahamika jina mwenye jinsi ya kiume.

Majeruhi katika ajali hiyo ni Ngeleja Mlima (36), Allen Gahanga (21), Sprime Kitanda (35), Fredrick Mgalula (36), Charles Mashauri (23), Novat Isaya (23) na Paulo Kayuki (25).

Miili ya marehemu imehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa na majeruhi wanaendelea na matibabu katika hospitali hiyo.

Alisema chanzo cha ajali ni uzembe wa dereva wa lori kujaribu kuyapita magari yaliyokuwa mbele, bila kuchukua tahadhari.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alithithibitisha kutokea kwa ajali hiyo.

Alisema basi hilo lilikuwa likitoka Mwanza kwenda Mbeya na dereva wake ni Emmanuel John Ng'wiguka (49) mkazi wa Buzuruga Mwanza .

TANGAZO

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30-09-2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 30/9/2021 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 30/6/2021 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 887 | 465 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 66 | 5 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 2,910 | 2,036 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 14,296 | 15,517 |
| 12 | Mali nyingine | 4,272 | 3,725 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 554 | 571 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **22,985** | **22,317** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 14,745 | 14,497 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 337 | 95 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,034 | 976 |
| 28 | Madeni | 2,586 | 2,686 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **18,705** | **18,257** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **4,280** | **4,060** |
| | | - | - |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | - |
| 32 | Akiba ya Mtaji | (5,278) | (5,278) |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 668 | 365 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 101 | 184 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| **37** | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **4,280** | **4,060** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,102 | 2,032 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,051 | 998 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 18.62% | 18.19% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 13.70% | 13.60% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 94.76% | 106.32% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 62.19% | 69.53% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 87.20% | 84.26% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 3.36% | 2.78% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.99% | 2.11% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-09-2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/9/21 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/6/20 | Limbikizo lamwaka sasa 30/9/21 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30/9/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,020 | 1,008 | 3,075 | 2,858 |
| 2 | Gharama za Riba | (200) | (277) | (661) | (660) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **819** | **731** | 2,414 | 2,198 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (53) | (51) | (235) | (51) |
| | | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 224 | 179 | 610 | 552 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | **180** | **137** | 553 | 410 |
| | 6.3 Gawio | | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 45 | 41 | 12 | 142 |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | **(687)** | **(568)** | **(2,120)** | (2,066) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (352) | (325) | (1,026) | (860) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (53) | (44) | (156) | (131) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (283) | (199) | (938) | (1,075) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **304** | 291 | 668 | 633 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (30) | (58) | (90) | (127) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **274** | 233 | 578 | 506 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **274** | **233** | **578** | **506** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 56 | 56 | 60 | 58 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 8 | 7 | 18 | 15 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 1.34% | 1.42% | 2.95% | 3.09% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 7.28% | 13.10% | 16.02% | 28.53% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 55.25% | 47.87% | 57.55% | 60.58% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 4.53% | 6.13% | 13.34% | 13.35% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho
kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30-09-2021
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Mwaka wa sasa** | | | | |
| | **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,887** | **(5,280)** | **87** | **3,694** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 668 | - | **668** |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| | Miamala na Wanahisa | - | - | - | - |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| | Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (83) | - | - | **(83)** |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,804** | **(4,612)** | **87** | **4,280** |
| | | | | | |
| | **Mwaka Uliopita 2019** | | | | |
| | Salio la mwanzo wa mwaka | 2,763 | (4,116) | 24 | **(1,329)** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 716 | - | **716** |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| | Miamala na wanahisa | 6,124 | - | - | **6,124** |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| | Tengo la ziada ya Jumla | - | (1,817) | - | **(1,817)** |
| | Mengineyo | - | (63) | 63 | - |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,887** | **(5,280)** | **87** | **3,694** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-09-2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/9/21 | Robo ya Mwaka iliyopita 30/6/21 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30/9/21 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 309/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 304 | 161 | 668 | 633 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | Hasara Katika Mali | 156 | 128 | 582 | 182 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,168 | (401) | (570) | (1,211) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 491 | 393 | (113) | (483) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | 88 | (91) | (90) | 246 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (547) | 52 | (675) | 764 |
| | Kodi Iliyolipwa | (30) | (30) | (90) | (160) |
| | Mengineyo (Bainisha) | (56) | (57) | (191) | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **1,573** | **154** | **(480)** | **(29)** |
| | | - | - | - | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana** | - | - | - | - |
| | **na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| | Gawio lililopokewa | (31) | (15) | (88) | (66) |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | **(31)** | **(15)** | **(88)** | **(66)** |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | - | - | - | - |
| | | - | - | - | - |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | (100) | - | (200) | (199) |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | 5,000 |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | (5) |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (83) | - | (83) | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (183) | | | |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **-** | **-** | **(283)** | **4,796** |
| | | - | - | - | - |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | - | - | - | - |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | - | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 1,359 | 139 | (850) | 4,701 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/ | 2,506 | 2,367 | 4,714 | 2,266 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/ | **3,864** | **2,506** | **3,864** | **6,967** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Philip Raymond<br>Meneja Mkuu | (Imesainiwa) | 30/Sep/2021 |
| Kelvin Mushi<br>Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | (Imesainiwa) | 30/Sep/2021 |
| Saleh S. Abdallah<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | (Imesainiwa) | 30/Sep/2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Prof. Dominicus Kasilo.<br>Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | (Imesainiwa) | 30/Sep/2021 |
| 2. Kitova Mungai<br>Mkurugenzi | (Imesainiwa) | 30/Sep/2021 |

## MUCOBA BANK PLC- CHARGES AND FEES- 2021

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account (GS09)** | |
| Account opening minimum amount | Free |
| Minimum operating balance | Free |
| Minimum Interest Bearing balance | N/A |
| Cash Withdrawal Fee | Refer cash withdrawal fee below |
| Credit Interest Rate | N/A |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 10,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Interest Rate | |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |
| Prematurity withdrawals | 10,000 |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | Rate |
|---|---|
| 3 months | 4% |
| 6 months | 5% |
| 12months | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs**10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 1,500 |
| Cash withdrawal- from Tzs 5,000,000 and above) | 0.08%, Max Tzs 150,000 |
| Account closure | 10,000 |
| Dormant account reactivation | 5,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,500 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Bank Statement Fee /page | 1,200 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balance Inquiry | 200 |
| Money Transfer | 15,000 |
| ATM card Cost | 15,000 |
| Searching Fee | 10,000 |
| Coins deposit fee | 10% |
| ATM card replacement | 10,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,300 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,300 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alart | 500 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |
| ATM Balance Inquiry | 200 |

**LOAN CHARGES AND COMMISION**

| S/NO | CHARGIES |
|---|---|
| 1. | -Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 20,000/= |

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL, UNITED VITANI

LIVERPOOL imeungana na Manchester United katika mbio za kutaka kumsajili kiungo wa Leeds na Timu ya Taifa ya England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 25, kwa ada ya pauni milioni 60. ***(Star)***

### RAPHINA ANUKIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imeingia katika mbio za kumsaka winga wa Leeds, Raphinha mwenye umri wa miaka 24, baada ya kupigiwa chapuo na Mbrazil mwenzie, Neymar. ***(Teamtalk)***

### BELLINGHAM SOKONI

LIVERPOOL ni moja ya klabu zilizoonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 18, kutoka Borussia Dortmund. ***(Sport1, via Sun)***

### OVERMARS MAMBO SAFI

MARC Overmars ataondoka Ajax na kuwa Mkurugenzi mpya wa soka wa Newcastle ifikapo Januari au Februari, mwakani. ***(De Telegraaf via Voetbal Primeur)***

### SOLSKJAER KUTAJIRIKA

MANCHESTER United italazimika kumlipa kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer fidia ya pauni milioni 7.5 kama itaamua kumtimua kazi kwa sasa. ***(Sun)***

### RONALDO AHITAJI KUSHINDA

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, alijaribu kuwakusanya na kuwashiwishi wachezaji wenzake kumuunga mkono Ole Gunnar Solskjaer. ***(Manchester Evening News)***

### WIRTZ AWINDWA EPL

KLABU ya Newcastle ilimfuatilia kiungo wa Bayer Leverkusen, Florian Wirtz, 18, wakati kinda huyo wa kimataifa wa Ujerumani alipokuwa dimbani Jumapili dhidi ya Cologne. ***(Bild)***

### DORTMUND YAJIPANGA IMARA

KLABU ya Borussia Dortmund ipo kwenye mawasiliano na Chelsea kuhusu hatima ya mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, winga Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 20, na winga wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 23. ***(Teamtalk)***

### SALAH, LIVERPOOL KUTETA

LIVERPOOL inapanga kuanza mazungumzo ya kuongeza mkataba na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah, 29. ***(Teamtalk)***

### EDWARDS KUONDOKA LIVER

MICHAEL Edwards ataondoka kwenye nafasi yake ya mkurugenzi wa soka wa Liverpool mwishoni mwa msimu huku bado Mwingereza huyo mwenye miaka 41 hajahusishwa na kazi yoyote kwa sasa. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# HATIMAYE BARCELONA YAMTIMUA KOEMAN

**●●● Ni kutokana na mwenendo mbaya wa timu tangu kuanza kwa msimu huu huku...**

**BARCELONA,** Hispania

RONALDO Koeman amefukuzwa na Barcelona baada ya klabu hiyo kuwa na mwanzo mbaya zaidi wa msimu wa 2021-22.

**Koeman alichukua nafasi ya Quique Setien, Agosti, mwaka jana lakini ameshindwa kuleta mabadiliko yoyote hapo Camp Nou wakati Barca ikiwa kwenye hali mbaya ya kifedha, iliyochangia Lionel Messi kwenda kujiunga na Paris Saint-Germain.**

Barca ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya mechi 10 na juzi Jumatano ilifungwa na Rayo Vallecano.

Kufungwa huko kulifuatiwa na kupoteza kwa mabao 2-1 mikononi mwa Real Madrid kwenye mchezo wa El Clasico, hali iliyosababisha mashabiki kuvamia gari la Koeman wakati akiondoka uwanjani.

Barca pia kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya imekuwa na kiwango kibaya, ikifungwa mechi mbili na kushinda moja.

Blaugrana hao walifungwa 3-0 na Bayern Munich na idadi kama hiyo na Benfica kwenye mechi za ufunguzi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, kabla ya kupata ushindi wa 1-0 kutoka kwa Dynamo Kiev.

Hiyo ni mara ya kwanza kwa Barca kupoteza mechi mbili za ufunguzi kwenye michuano hiyo, huku kufungwa na Benfica pia kulifanya timu hiyo kupoteza mechi mfululizo kwenye msimu mmoja kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2000-01.

Kocha Louis van Gaal pekee aliyepoteza mechi nyingi mfululizo (tano) kabla ya Koeman (tatu).

"FC Barcelona imeachana rasmi na kocha Ronald Koeman na inamshukuru kwa mchango wake wakati akikinoa kikosi cha kwanza," ilisomeka taarifa ya klabu hiyo.

"Rais wa klabu, Joan Laporta, amemjulisha yeye kuhusu uamuzi wa kuachana naye baada ya kipigo kutoka kwa Rayo Vallecano.

"FC Barcelona inamtakia kila la heri katika maisha yake mapya na inamshukuru kwa mchango wake."








# POGBA AKANUSHA KUMTUKANA SOLSKJAER

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Paul Pogba, amekanusha madai ya kumtusi kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer baada ya kipigo cha Jumapili cha mabao 5-0 kutoka kwa Liverpool pale Old Trafford.

Ilikuwa siku mbaya kwa Mfaransa huyo wakati akiachwa kwenye kikosi cha kuanza hadi kipindi cha pili, akishuhudia timu yake ikichapwa mabao manne kipindi cha kwanza na yeye akaingia akitokea benchi kipindi cha pili. Pogba alicheza kwa dakika 15 tu kabla ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu na mwamuzi, Anthony Taylor baada ya kumchezea vibaya, Naby Keita.

Mchezaji huyo wa zamani wa Juventus amekuwa kwenye wakati wa kupanda na kushuka akiwa na United tangu alipotua akitokea Italia mwaka 2016, na uvumi umekuwa ukizagaa kuhusu majaliwa yake huku mkataba wake ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Pia kumekuwa na maswali kuhusu mahusiano yake na Solskjaer, pamoja na wachezaji, hasa baada ya mashetani wekundu hao kupoteza mchezo huo wa nne huku wakitoka sare moja katika mechi tano zilizopita.

Hata hivyo, Pogba aliandika kupitia ukurasa wake wa Twitter juzi Jumatano kwamba, habari iliyochapishwa na gazeti la Sun kudai alimtukana kocha wake kwenye vyumba vya kubadilishia nguo ni za uongo.



## *Allegri: Hali yetu mbaya*

**TURIN,** Italia

MASSIMILIANO Allegri aliachwa kachanganyikiwa wakati Juventus ikikumbana na kichapo kutoka kwa Sassuolo, katika mechi iliyochezwa juzi Jumatano.

Juventus ilipoteza kwa mabao 2-1 pale kwenye Uwanja wa Allianz dhidi ya Sassuolo. Bianconeri hao walisawazisha bao la Davide Frattesi, wakati Weston McKennie akiwarudisha mchezoni zikiwa zimebaki dakika 14 mpira kumalizika.

Maxime Lopez alifunga bao la ushindi kwa Sassuolo dakika ya 95, na kuifanya Juve kufungwa mchezo wa tatu wa Serie A katika mechi 10 msimu huu.

Lilikuwa bao la 13 kufungwa na Juve msimu huu yakiwa mengi zaidi tangu msimu wa 1988-89.

"Tumekuwa kwenye wakati mgumu na hali ilikuwa tofauti na tulivyotarajia," alisema Allegri aliwaambia waandishi wa habari.

"Wakati unaposhindwa kupata matokeo, tumepoteza pointi muhimu sana hivyo tunatakiwa kujipanga upya."



## HABARI MICHEZO


,207,580

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/10/21 | 17:00 | Watford vs Southampton | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 02. 30/10/21 | 17:00 | Burnley vs Brentford | 2.80 | 3.20 | 2.60 |
| 03. 30/10/21 | 17:00 | Derby vs Blackburn | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 04. 30/10/21 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 05. 30/10/21 | 18:00 | Metz vs St Etienne | 2.59 | 3.34 | 2.64 |
| 06. 30/10/21 | 19:30 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.79 | 3.38 | 2.49 |
| 07. 30/10/21 | 19:30 | Valencia vs Villarreal | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 31/10/21 | 15:00 | Angers vs Nice | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 09. 31/10/21 | 16:00 | Cadiz CF vs Mallorca | 2.67 | 2.97 | 2.92 |
| 10. 31/10/21 | 17:00 | Bordeaux vs Reims | 2.43 | 3.19 | 2.94 |
| 11. 31/10/21 | 17:30 | Augsburg vs Stuttgart | 2.80 | 3.30 | 2.47 |
| 12. 31/10/21 | 19:30 | Aston Villa vs West Ham | 2.77 | 3.42 | 2.49 |
| 13. 31/10/21 | 22:45 | Roma vs AC Milan | 2.49 | 3.42 | 2.77 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 29 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 1279 | Polissya Zhytomyr vs FC Nyva Ternopil | 1.85 | 3.34 | 3.87 |
| 15:50 | 1376 | Dibba Al Fujairah vs Al-Hamriyah | 2.04 | 3.86 | 2.84 |
| 16:00 | 1565 | Mbeya Kwanza FC vs Biashara United | 2.50 | 2.75 | 3.35 |
| 16:00 | 1852 | Sectzya Nes Ziona vs Maccabi Bney Reine | 2.31 | 3.27 | 3.02 |
| 16:00 | 2010 | El Fahem vs Hapoel Rishon Lezion | 2.34 | 3.21 | 3.01 |
| 16:00 | 3385 | Kfum Oslo vs Aalesunds | 3.18 | 3.56 | 1.98 |
| 16:00 | 3566 | Hapoel Afula vs Hapoel Kfar Saba | 5.94 | 3.81 | 1.56 |
| 17:00 | 1482 | US Biskra vs JS Saoura | 2.67 | 2.86 | 2.67 |
| 17:00 | 1945 | JS Kabylie vs ES Setif | 2.52 | 3.00 | 2.71 |
| 19:00 | 1142 | KMC vs Kagera Sugar | 2.14 | 2.69 | 3.84 |
| 19:00 | 1693 | Cracovia vs Radomiak Radom | 2.12 | 3.19 | 3.24 |
| 19:00 | 2428 | IK Start vs Strommen | 1.40 | 4.62 | 5.97 |
| 19:00 | 4016 | Stjordals vs Blink-Jerv | 3.32 | 3.51 | 1.94 |
| 19:00 | 4462 | Zenit St Petersburg vs Dinamo Moscow | 1.46 | 4.42 | 5.89 |
| 19:00 | 4992 | Sandnes Ulf vs Sogndal | 2.49 | 3.45 | 2.44 |
| 19:00 | 5211 | Raufoss vs Ranheim | 1.90 | 3.86 | 3.18 |
| 19:30 | 1625 | SV Horn vs Wacker Innsbruck | 5.19 | 4.23 | 1.49 |
| 19:30 | 1687 | FC Liefering vs Vorwarts Steyr | 1.14 | 7.13 | 12.52 |
| 19:30 | 5473 | SV Lafnitz vs Rapid Vienna II | 1.73 | 3.72 | 3.96 |
| 20:00 | 2069 | Trabzonspor vs Caykur Rizespor | 1.33 | 5.13 | 7.70 |
| 20:00 | 4436 | Lyngby vs FC Helsingor | 2.28 | 3.52 | 2.65 |
| 20:00 | 4575 | GD Chaves vs CD Trofense | 1.74 | 3.52 | 4.40 |
| 20:15 | 2006 | Sccm Chabab Mohammedia vs Hassania Agadir | 2.12 | 3.14 | 3.24 |
| 20:30 | 1829 | Botosani vs Farul Constanta | 2.64 | 3.03 | 2.69 |
| 21:00 | 3264 | Den Bosch vs Jong Utrecht | 2.50 | 3.52 | 2.50 |
| 21:00 | 3317 | Ullensaker/Kisa vs Ham-Kam | 4.34 | 3.86 | 1.64 |
| 21:00 | 4123 | FC Volendam vs Dordrecht | 1.18 | 7.05 | 10.78 |
| 21:00 | 5985 | Emmen vs VVV Venlo | 1.45 | 4.49 | 5.86 |
| 21:30 | 2637 | Stal Mielec vs Lech Poznan | 5.38 | 4.04 | 1.50 |
| 21:30 | 3080 | Korona Kielce vs OKS Odra Opole | 1.68 | 3.66 | 4.34 |
| 21:30 | 3240 | Longford Town vs St Patricks | 7.14 | 4.34 | 1.37 |
| 21:30 | 4105 | Santiago Wanderers vs CD Palestino | 3.09 | 3.38 | 2.08 |
| 21:30 | 4198 | Hoffenheim vs Hertha BSC | 1.69 | 4.08 | 4.38 |
| 21:30 | 5833 | Neuchatel Xamax vs FC Winterthur | 2.16 | 3.43 | 2.90 |
| 21:45 | 1329 | Shelbourne vs UCD Dublin | 1.74 | 3.75 | 3.85 |
| 21:45 | 2065 | QPR vs Nottingham | 2.08 | 3.39 | 3.29 |
| 21:45 | 2957 | Derry City vs Bohemians FC | 2.60 | 3.17 | 2.50 |
| 21:45 | 3273 | Sligo Rovers vs Drogheda Utd | 2.09 | 3.17 | 3.27 |
| 21:45 | 3438 | Cabinteely vs Treaty United | 3.16 | 3.45 | 2.02 |
| 21:45 | 4171 | Oostende vs Mechelen | 2.61 | 3.50 | 2.46 |
| 21:45 | 4932 | Dundalk FC vs Waterford Utd | 1.60 | 3.81 | 4.72 |
| 21:45 | 5297 | Wexford Youths vs Bray Wanderers | 6.75 | 4.63 | 1.36 |
| 21:45 | 5621 | Cork City vs Galway United | 2.93 | 3.37 | 2.16 |
| 22:00 | 1194 | Almeria vs Leganes | 1.81 | 3.34 | 4.42 |
| 22:00 | 4260 | CD Linares vs Barcelona B | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 22:00 | 4613 | Rayo Majadahonda vs Racing Ferrol | 2.11 | 3.03 | 3.37 |
| 22:00 | 4802 | Paris St Germain vs Lille | 1.42 | 4.80 | 6.65 |
| 22:00 | 5066 | Aberystwyth Town vs Flint Town United | 3.66 | 3.56 | 1.83 |
| 22:00 | 5931 | Real Sociedad B vs Las Palmas UD | 2.70 | 3.00 | 2.65 |
| 22:15 | 1639 | FC Arouca vs Tondela | 2.04 | 3.30 | 3.55 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# CHELSEA WAPEWA OFA KWA DE LIGT



**TURIN,** Italia

KLABU ya Chelsea imepewa ofa na nafasi ya kumsajili beki wa kati wa Juventus, Matthijs de Ligt, kwa mujibu wa Goal.com imeandika.

Juventus ipo katika hali mbaya kiuchumi kwa sasa na klabu hiyo ya Serie A imepanga kupunguza baadhi ya wachezaji wenye mishahara mirefu akiwamo de Ligt.

Ni timu chache kwa sasa ikiwamo Chelsea ambazo zinaweza kukamilisha usajili wa beki huyo kutokana na vilabu vingi kuyumba kiuchumi kwa sababu ya janga la Covid-19.

Ripoti hiyo imesema De Ligt mwenyewe yupo tayari kuondoka kwa miamba hao, kwa sababu hana furaha katika kikosi hicho. Awali iliripotiwa De Ligt anataka kuondoka Juve na Barcelona ndio iliyokuwa ikitajwa kuwa na nafasi kubwa ya kumsajili.

Chelsea bado inapambana kuongeza mikataba ya mabeki wake wanne, Andreas Christensen, Antonio Rudiger, Thiago Silva na Cesar Azipilicueta ambao mikataba yao inaisha katika majira ya kiangazi 2022.




Mshindi wa Jackpot bonus, Respicius Baitwa, kutoka Mtwara akiwa na mfano wa hundi ya Sh. milioni 9.6 mara baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Wengine walioshinda Jackpot bonus ni Mustafa Athumani na Moses Kalao. Jackpot ya SportPesa wiki hii ni Sh. milioni 619.2. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Kepa kamili kubeba mikoba ya Mendy*

**LONDON,** England

KEPA Arrizabalaga amesema yupo tayari kuchukua mikoba ya Edouard Mendy wakati atakapokwenda kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika, hapo Januari mwakani.

Kepa ambaye amecheza michezo minne katika msimu huu na mchezo wa mwisho dhidi ya Southampton ambao aliibuka shujaa baada ya kuokoa mikwaju ya penalti na kuisaidia Chelsea kufuzu hatua ya robo fainali.

"Twende hatua kwa hatua na tutaona kitakachotokea, kama akienda kwenye michuano ya AFCON, namtakia kila la heri na nitakuwa tayari lakini kuna muda mrefu bado," alisema Kepa akinukuliwa na Bt Sport.

Mendy, kipa chaguo la kwanza kwa sasa anatarajia kwenda kwenye michuano ya AFCON kuiwakilisha timu yake ya Senegal ambapo michuano hiyo itachukua karibia wiki nne.

"Bila shaka nahitaji kucheza mara kwa mara, mchezo wangu wa mwisho pia ulikuwa kwenye kombe, ni mwezi sasa umepita.

"Sio rahisi muda mwingine kuingia na kujihisi sawa kama mchezaji anyecheza kila wiki, lakini najitahidi kuwa tayari, kufanya mazoezi kwa juhudi na kushirikiana na timu."

# Michezo

Ijumaa Oktoba 29, 2021

Nipashe




Hatimaye Barca yamtimua Koeman UKURASA 21



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Bernard Morrison (kulia), akipambana kumtoka mchezaji wa Polisi Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga SC heshima itabaki pale pale

**Na Mwandishi Wetu**

TUKO kamili kuendeleza heshima! Hayo ni maneno ya Yanga kuelekea mchezo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Azam FC utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia gazeti hili wachezaji wa timu hiyo wanaendelea vyema na wako tayari kupambana kwa ajili ya kuondoka na ushindi katika mchezo huo.

Saleh alisema kila mchezaji wa Yanga anafahamu umuhimu wa mechi hiyo na wamejiandaa kuendelea kuwapa furaha wanachama na mashabiki wao.

"Malengo yetu ni kutwaa ubingwa, na ili uwe bingwa ni lazima upate pointi nyingi, tunahitaji ushindi ili tuendelee kujiimarisha katika msimamo wa ligi, tunajua haitakuwa mechi rahisi kwa sababu wenzetu pia wamejipanga na wana kikosi imara," Saleh alisema.

Yanga ndio vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16, ikiwa na pointi tisa sawa na Polisi Tanzania wakati watani zao na mabingwa watetezi Simba wenye pointi saba wako katika nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Kikosi hicho cha Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi kimekaa kileleni kwa sababu ya kuwa na uwiano mzuri wa mabao ya kufunga, imetikisa vyavu za wapinzani mara nne na haijaruhusu bao kwenye lango lake.

Yanga ndio ilikuwa ya kwanza kwa upande wa timu za Tanzania Bara kuondolewa kwenye mashindano ya kimataifa kwa kukubali kichapo mara mbili kutoka kwa Rivers United ya Nigeria.

# Simba mwendo wa vishindo

## Hitimana asema michuano ya CAF sasa si...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuendelea kuwapo katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba ya jijini Dar es Salaam wamesema kwa sasa kipaumbele chao ni kuona wanatetea ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambao wanaushikilia.

**Kauli hiyo ya Simba imetolewa baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Polisi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi.**

Jumapili iliyopita Simba ilitolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Jwaneng Galaxy ya Botswana na sasa itacheza mechi ya mtoano na Reds Arrows ya Zambia ambapo mshindi atatinga hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Thierry Hitimana, alisema wameamua kuweka nguvu kwenye mechi za Ligi Kuu kwa sababu wanahitaji kutwaa ubingwa kwa mara ya tano mfululizo na wameweka kando mikakati ya mchezo wao dhidi ya Red Arrows.

Hitimana alisema nguvu na akili zao zote zitakuwa katika kutafuta pointi tatu kwenye kila mechi ya Ligi Kuu Tanzania na si kitu kingine.

"Tumeona ratiba na tumemfahamu mpinzani wetu tutakayekutana naye katika Kombe la Shirikisho, hatuwezi kusema lolote kuhusu Reds Arrows kwa sababu mechi iko mbali, kipaumbele chetu ni Ligi Kuu," alisema Hitimana.

Aliongeza hawezi kuanza kuufikiria mchezo huo kwa sababu bado ana mechi nyingine mbili 'ngumu' ambazo ni dhidi ya Coastal Union na Ruvu Shooting ambazo wanahitaji kuondoka na pointi zote sita katika michezo hiyo.

"Kwa sasa hatuwezi kuizungumzia Reds Arrows kwa sababu tuna kibarua kigumu mbele yetu kuhakikisha tunashinda mechi za ligi kuu zilizopo mbele yetu ikiwamo dhidi ya Coastal Union na Ruvu Shooting ambazo ziko karibu."

"Tunatambua ligi msimu huu kuna ushindani mkubwa, tumerejea uwanjani kufanyia kazi madhaifu yetu yaliyotokea katika michezo iliyopita ikiwamo tuliocheza jana (juzi ) dhidi ya Polisi Tanzania," alisema Hitimana.

Aliongeza malengo makubwa ya Simba ni kufanya vizuri katika michezo yote iliyopo mbele yao na itakapokaribia mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika wataanza maandalizi yake.

Kuhusu mechi ya juzi, Hitimana alisema walicheza kwa 'presha kubwa' iliyotokana na 'mawenge' waliyokuwa nayo baada ya kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ningependa kuwapongeza na kuwashukuru wachezaji wangu kwa kupambana na kupata pointi tatu muhimu. Katika mchezo wa jana (juzi), tulikuwa na wapinzani wawili, wa kwanza ni sisi wenyewe pamoja na Polisi Tanzania, kikubwa tumepata ushindi na kufikia malengo katika mchezo huu," alisema kocha huyo.

Alisema mabadiliko ya wachezaji wanne katika kikosi kilichoanza juzi yalitokana na baadhi ya nyota wake wanaocheza katika eneo la kiungo kuwa majeruhi na ndio maana alibadilisha kikosi.

"Ukiangalia Taddeo Lwanga ni majeruhi aliumia kwenye mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy, na Jonas Mkude hakuwa fiti asilimia 100 ndio maana tumefanya mabadiliko yale kikosini ingawa nilitamani kuanza na washambuliaji wawili, lakini kikubwa tunafurahi kwa ushindi tuliopata," kocha huyo alisema.

Simba inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwakaribisha Coastal Union katika mechi nyingine ya Ligi Kuu itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >